**UTOUH** ataja kiini serikali kununua kwa bei zilizopitiliza
UKURASA 4

**MGAMBO** waliotaka kukamata mifugo kijijini watimuliwa
UKURASA 5



**RAMAPHOSA** avuka mtihani, aapishwa urais awamu ya pili
UKURASA 19



**MAN CITY KUFUNGUA EPL NA CHELSEA MSIMU WA 2024/25.**
UKURASA 22


# Nipashe

Alhamisi Juni 20, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581713

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


## MAUAJI MWENYE UALBINO

# Paroko, mganga na baba mbaroni

**WADAIWA** kukutwa na viungo wakisaka mteja... *Endelea ukurasa 2*



DCP David Misime

# Simbachawene: Kashfa zimezidi Ardhi, washtakiwe kwa makosa jinai

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amesema moja kati ya maeneo yanayoongoza kwa kulalamikiwa kwenye utumishi wa umma ni ardhi na yeye akiwa mmoja wa waliovamiwa

ENDELEA UKURASA WA 3



UKURASA WA 17

## VIONGOZI WA MABUNGE DUNIANI KUKUTANA ZANZIBAR

VIONGOZI wa Kamati wa Umoja wa Mabunge Duniani wamekutana...

UKURASA WA 23

## JOB AMWANGUKIA KOCHA MOROCCO

HATIMAYE beki wa timu ya Yanga, Dickson Job, amemuomba radhi Kocha wa Timu y...



# Samia atoa ndege msiba wa RAS K'njaro

UKURASA 2



## MAFURIKO JANGWANI

Baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam wakitumia mkokoteni kuvushwa kwenye maji yaliojaa katika eneo la Jangwani, kutokana na mvua kubwa iliyonyesha jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**MICHEZO** **YANGA: TUMEWALIPA WALIOTUBURUZA FIFA** UK 24

**MAONI, KATUNI UK.6**




Meneja Miradi wa Umoja wa Ulaya (EU) anayeshughulikia Miundombinu na Uwekezaji, Alessandro Trevisan (kushoto), akiwasilisha mada jijini Dar es Salaam jana, wakati wa mkutano wa EU na wadau wa fedha uliojadili fursa na upatikanaji wa pesa za kusaidia miradi ya wanawake na vijana wajasiriamali wadogo na wa kati. **PICHA: JOHN BADI**

MAUAJI MWENYE UALBINO

# Paroko, mganga, baba wakamatwa

**Na Romana Mallya**

WATU tisa wanashikiliwa na Jeshi la Polisi wakidaiwa kukutwa na viungo vinavyodhaniwa vya mwenye ualbino mkoani Kagera wakiwa wamevihifadhi katika vifungashio vya plastiki wakitafuta mteja.

Kati yao, wamo Paroko Msaidizi wa Bugandika, Elipidius Rwegoshora, mganga wa jadi, Desideli Evalist, mkazi wa Nyakahama na Novart Venant, ambaye ni baba mzazi wa mtoto Asimwe Novath (2), aliyechukuliwa mikononi mwa mama yake Mei 30 mwaka huu na watu wasiojulikana na mwili wake kugundulika baada ya siku 19, akiwa ameuawa.

Mwili wa mtoto huyo ambao ulikutwa baadhi ya viungo vikiwa vimenyofolewa huku ukiwa kwenye mfuko wa sandarusi, uliopolewa Jumatatu katika karavati linalopitisha maji katika barabara iliyoko Luhanga kwenda Kijiji cha Makongora, mkoani Kagera.

Katika taarifa Jeshi la Polisi iliyotolewa jana na msemaji wa jeshi hilo nchini, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP) David Misime, ilibainisha kuwa baada ya tukio hilo, jeshi kwa kushirikiana na raia wema, lilifanya msako mkali kuanzia Mei 31 mwaka huu hadi usiku wa kuamkia jana na kukamata watuhumiwa tisa.

Misime alisema katika taarifa yake hiyo kuwa watuhumiwa hao wamekamatwa wakiwa wamevihifadhi viungo vinavyodhaniwa ni vya mtoto Asimwe, wakiwa wamevihifadhi katika vifungashio vya plastiki wakitafuta mteja.

"Watuhumiwa waliokamatwa ambao walieleza jinsi walivyoshiriki katika tukio ni baba mzazi wa mtoto, mganga wa jadi na Paroko Msaidizi wa Parokia ya Rugandika, Rwegoshora, ambaye anadaiwa kumfuata na kumshawishi baba mzazi wa mtoto ili wafanye biashara ya viungo vya binadamu.

"Pia anatuhumiwa kuwa ndiye aliyemtafuta mganga wa jadi na kumlipia gharama zote za uganga. Watuhumiwa wengine ni Dastan Kaiza, mkazi wa Bushagara na Faswiru Athuman, mkazi wa Nyakahama (wote wilayani Muleba).

"Wengine ni Gozibert Alikadi, mkazi Nyakahama Kamachumu, Rwenyagira Burkadi, mkazi wa Nyakahama Kamachumu, Ramadhani Selestine, mkazi wa Kamachumu na Nurduni Hamada, mkazi wa Kamachumu," alisema.

Misime alisema Jeshi la Polisi linatoa onyo kwa watu wanaoendekeza imani za kishirikina ikiwamo kupiga ramli chonganishi wakiaminishana kwamba wanaweza kupata utajiri kwa njia za kishirikina kuacha tabia hiyo.

**Mwili wa mtoto huyo ambao ulikutwa baadhi ya viungo vikiwa vimenyofolewa huku ukiwa kwenye mfuko wa sandarusi, uliopolewa Jumatatu katika karavati linalopitisha maji katika barabara iliyoko Luhanga kwenda Kijiji cha Makongora, mkoani Kagera.**

"Waache kudanganya kwamba kuna utajiri unaopatikana kwa kumiliki viungo vya binadamu mwenye ualbino, kwani si kweli kwa kuwa kama ingekuwa hivyo, familia zenye watoto au ndugu wenye ualbino wangekuwa na utajiri mkubwa, badala yake tunaona wakiishi maisha ya kawaida kama sisi wengine," alisema.

Misime aliongeza kuwa wanaofanya vitendo hivyo wanapaswa kutambua ni uhalifu uliopitiliza katika karne hii ya maendeleo ya sayansi na teknolojia kutenda ukatili huo, kwa kuwa yeyote anayefanya na anayeshiriki katika uhalifu wa aina hiyo, lazima atakamatwa kwa kuwa vitendo hivyo havina baraka za Mwenyezi Mungu wala sheria za nchi.

"Ni vitendo vya aibu kwa anayefanya na kwa familia yake pia, wanalifedhehesha taifa. Watu wenye mawazo hayo waachane nayo, wafanye kazi halali, watoke jasho na ndiyo siri ya kufanikiwa katika maisha na si kuendeleza ushirikina na kupiga ramli chonganishi," alisema.

Juzi Rais Samia Suluhu Hassan alisema kuwa kifo cha mtoto mwenye ualbino kimemgusa, huku akitaka washiriki wa Kongamano la Maendeleo ya Sekta ya Habari, alilokuwa analifungua, kusimama kwa muda na kuomba kwa ajili ya kundi hilo.

***SOMA TAARIFA ZAIDI KUHUSU SUALA HILI UKURASA WA 5**

## Rais Samia atoa ndege kusafirisha mwili wa RAS

**Na Waandishi Wetu,** MOSHI

RAIS Samia Suluhu Hassan, ametoa ndege maalum itakayoubeba mwili wa aliyekuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro (RAS), Dk. Tixon Nzunda (56), kwenda nyumbani kwake Goba, jijini Dar es Salaam leo kwa ajili ya mazishi.

Aidha, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, amemwelezea marehemu Dk. Nzunda, alikuwa kiongozi wa umma mwadilifu katika kuwatumikia wananchi na kila mara alikuwa na hofu ya kuwatanguliza wananchi.

Dk. Nzunda na dereva wake, Alphonce Edson (54), walipoteza maisha Juni 18, mwaka huu, saa 8:30 mchana katika eneo la Mjohoroni (Palestina), Kata ya KIA, Wilaya ya Hai, baada ya gari lake aina ya Toyota Land Cruiser VXR, kugongana uso kwa uso na lori la kubeba nishati ya gesi safi, mali ya Kampuni ya Orange Gas.

Lori hilo lenye namba za usajili T 655 ABY, aina ya Scania lilikuwa likitokea Arusha kwenda Moshi.

Jana Dk. Mpango akiwa katika makazi ya viongozi wa serikali eneo la Shanty Town katika Mji wa Moshi, alikokwenda kutoa salamu za rambirambi na kumfariji mjane wa Dk. Nzunda, alisema anamkumbuka vizuri marehemu, kwa kuwa alipokuwa Waziri wa Fedha, alikuwa anakaa naye.

"Nilishtuka kidogo maana jana (juzi), niliondoka nyumbani saa tisa alasiri, na sikuwa nimepata habari yoyote. Nilipofika kwenye Uwanja wa Ndege wa Dodoma, ndipo nilipo arifiwa kwamba mwenzetu ametangulia kupitia ajali mbaya pale karibu na KIA; na alikuwa anakuja kunipokea. Ni jambo gumu, lakini tumuombee mwenzetu.

...Nimemwomba Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, anifikishie salamu za pole kwa familia ya dereva wake, ambaye alifariki katika ajali ile. Natamani sana ningefika, lakini Mkuu wa Mkoa ataenda kutuwakilisha."

"Nilikuwa nakaa naye sana marehemu (Dk. Nzunda), akiwa Ofisi ya Waziri Mkuu, kwenye vikao vyetu vya utatu na wafanyakazi; ambapo alikuwa mtu makini sana na mpole.

"Kwa upande wa serikali tukio hili limetuumiza sana. Kwa niaba ya serikali na mimi mwenyewe, Rais yupo safarini, tunasema poleni sana na niwashukuru kwa moyo wenu toka tukio hili litokee; mmekuwa pamoja na familia na huu ndio Utanzania ninaoufahamu."

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alisema Juni 21 saa 4:00 asubuhi mwili wa Dk. Nzunda, utapelekwa nyumbani kwake Shanty Town na kufanyiwa ibada fupi, wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro watapata fursa ya kuuaga.

"Baadaye saa 10:00 jioni, mwili huo utasafirishwa kwa ndege maalum kuelekea nyumbani kwake jijini Dar es Salaam (Goba), kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA). Utakapofikishwa Dar es Salaam mwili huo utalala nyumbani hapo, ukimsubiria mtoto wake aliyeko nchini India, anayetarajiwa kufika Ijumaa saa 3:00 asubuhi," alisema maziko yatafanyika Juni 22.

Aidha, alisema mwili wa dereva wake, Alphonce Edson (54) unatarajiwa kuzikwa Julai 24, nyumbani kwake Mabogini Chekereni.

**RAIS SAMIA AMTUMIA POLE RC**

Rais Samia Suluhu Hassan amemtumia salamu za rambirambi Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, kutokana na kifo hicho.

Taarifa ya Ikulu iliyotolewa na Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais-Ikulu, Sharifa Nyanga, ilisema Rais Samia ametoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu.

**Imeandikwa na Godfrey Mushi na Mary Mosha**

# Simbachawene kula sahani na wavamizi ardhi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amesema moja kati ya eneo linaloongoza kwa kulalamikiwa kwenye utumishi wa umma ni ardhi na yeye akiwa mmoja wa waliovamiwa pamoja na kuwa na hatimiliki.

Simbachawene alibanisha hayo jana jijini hapa, wakati akifungua maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma inayotarajiwa kufika kilele chake Juni 23, mwaka huu.

Alisema hivi sasa kwenye utumishi wa umma sekta inayoongoza kwa malalamiko ni ardhi hali ambayo inahitaji serikali kuwekeza nguvu kubwa kukomesha hali hiyo.

"Hivi sasa eneo ambalo linalalamikiwa sana nchini katika utumishi wa umma ni ardhi kila mtu ana malalamiko hadi makatibu wakuu, wakurugenzi leo hii ukisema wenye malalamiko ya ardhi watoke mbele na wao watatoka.

"Inabidi tuunganishe nguvu kukomesha suala hili kwani hali ni mbaya katika sekta ya ardhi mimi mwenyewe hapa ninayo hatimiliki ya ardhi, lakini bado eneo langu limevamiwa sasa kama hatutachukua hatua ipo siku tutasikia na hati ya mheshimiwa Rais imevamiwa," alisema Simbachawene.

Alisema, ipo haja kwa serikali kuona namna mbadala ya kushughulikia migogoro ya ardhi kwa kuwashitaki kwa makosa ya jinani badala ya madai watumishi wa umma ambao wamekuwa wakihusika kuchochea hali hiyo.

"Hawa watumishi ambao wamekuwa wakihusika kuzalisha migogoro hii inabidi tuwachukulie hatua kwa makosa ya jinai ili wafungwe badala ya kuendelea kuwafungulia madai hii inawafanya kila siku wahalifu hawa kuonekana wao ndio washindi na wanaendelea kutucheka sisi," alisisitiza Simbachawene.

Alisema moja kati sababu zinazochangia Wizara ya Ardhi kuwa na migogoro mingi ni pamoja na watumishi wake kukiuka sheria, kughushi nyaraka na pia uhaba wa watumishi kwa kuwa wengi wao ni wa mkataba.

"Mimi waziri sioni kama ni afya kila mtu kufanya kazi moja ya kutatua migogoro ya ardhi, yaani unakuta diwani anatatua mgogoro wa ardhi, mkuu wa mkoa, waziri hata viongozi wakuu wa nchi wanatatua mgogoro wa ardhi, ipo haja kwa wale wanaovunja sheria kuwachukulia hatua kali," alisema.

Aidha, alitoa maagizo matano ambayo yatasaidia kuboresha utumishi wa umma ikiwamo watendaji wote ambao bado hawajajisajili kwenye mfumo wa kupima utendaji kazi kufanya hivyo mara moja.



"Watendaji na watumishi wa umma pia watumie mifumo ya Teknolijia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambayo imeanzishwa na serikali kuwawahudumia wananchi ambao wamekuwa wakilalamika kukosa huduma, pia kuwasilisha tathmini ya maadhimisho hayo na kutoa mrejesho," alisema.

Simbachawene, pia alitoa tahadhari kwa watumishi wa umma ambao wameshindwa kwenda na kasi ya serikali ya awamu ya sita kujitathmini ili waweze kutekeleza maagizo yanayotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Awali, Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwan Kikwete, alisema lengo la maadhimisho hayo ni pamoja na kutumia wiki hiyo kutoa huduma moja kwa moja kwa jamii.

Alisema, lengo jingine ni kutoa elimu kwa umma kuhusu mambo mbalimbali yanayofaywa na wizara mbalimbali pamoja na kuonyesha ubunifu na kupokea maoni kutoka kwa jamii kuhusu utoaji huduma.

Nao baadhi ya washiriki katika maonesho hayo akiwamo Ofisa wa kitengo cha huduma kwa wateja, Fatma Bororo, TANESCO makao makuu, alisema wanaendelea kutekeleza maagizo ya serikali ya kutumia mifumo kuhudumia wananchi.

Alisema hivi sasa wameanzisha namba ya kutoa huduma kwa wateja ambao wakitumia simu zao watapata majibu ya kero mbalimbali zinazowakabili.

"Lakini pia hivi sasa tupo katika maboreshoa ya mita za LUKU ambapo mteja akinunua umeme atapata makundi matatu ya tokeni na kuingiza kundi moja moja hadi mwisho atakuwa tayari amekamirisha maboresho hayo, zoezi hili tumeanza na kanda ya ziwa, badaye nyanda za juu kusini na tunataraji ifikapo Novemba mwaka huu kukamilisha nchi nzima," alisema Bororo.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala.
Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

HABARI KITAIFA

# Utouh ataja siri serikali kununua bidhaa kwa bei zaidi ya soko

**Na Mwandishi Wetu**

MDHIBITI na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) wa zamani, Ludovick Utouh amesema uchelewaji malipo kwa wazabuni unachangia serikali kununua bidhaa au huduma kwa bei kubwa kulinganisha na iliyoko sokoni.

Amesema wazabuni hulazimika kuweka bei kubwa kuliko ya bei ya sokoni wanapoomba zabuni serikalini kwa kuwa serikali hailipi kwa wakati.

Utouh aliyekuwa CAG nchini kwa miaka minane kuanzia 2006 hadi 2014, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam, wakati Taasisi ya WAJIBU anayoiongoza, ilipozungumzia Mkutano wa Kimataifa wa Uwazi na Uwajibikaji (ITAC 2024) uliopangwa kufanyika jijini Arusha Agosti 6 na 7 mwaka huu.

Alisema, "Haijalishi hata ikikaa kwa miaka mitano, serikali haikulipi kwa riba, inakulipa kilekile. Tunajua thamani ya fedha ya mwaka juzi si sawa na mwaka huu, pia ya mwaka huu si sawa na miaka itakayokuja. Kwahiyo, tenda zote waombaji wanataja dau kubwa kwa kuwa hawana uhakika wa kulipwa kwa wakati."

Utouh aliongeza, "Kama wamekufanyia kazi, lipa leo, lakini mtu anakufanyia kazi leo unakuja kulipa mwaka keshokutwa... bidhaa ya Sh. 3,000 kibiashara, nitalazimika mimi mzabuni niweke bei kubwa zaidi kwa sababu haitalipwa kwa wakati, ninakwenda mbele na hili ndilo tatizo kubwa, halitaisha kwa sababu ya ile thamani ya fedha inakosekana kwa mwenendo huu wa serikali."



**"Ili kuboresha michakato ya ununuzi wa umma ni muhimu kuhakikisha kunakuwapo thamani ya fedha katika ununuzi wa umma na kuwapo ukuzaji uwajibikaji wa kifedha katika sekta ya umma," alisema.**

**ITAC 2024**

Kuhusu ITAC 2024, Meneja Programu za Utafiti na Miradi wa Taasisi ya WAJIBU, Moses Kimaro, alisema jana kuwa mkutano wa mwaka huu una dhima ya kuchochea mifumo bora ya ununuzi wa umma kwa maendeleo endelevu Afrika.

Alisema kuwa mwaka huu wamejikita katika ununuzi wa umma ambao unachukua sehemu kubwa ya matumizi ya serikali zote barani Afrika, zaidi ya asilimia 70 ya bajeti zake.

Kimaro alisema kuwa taarifa za wakaguzi wa nchi mbalimbali barani zinaonesha kuwa kupitia mifumo ya ununuzi wa umma, kumekuwa na dosari za vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa fedha za umma ambavyo vinachangia kuzipunguzia serikali uwezo wa kifedha kuletea wananchi maendeleo.

"Ili kuboresha michakato ya ununuzi wa umma ni muhimu kuhakikisha kunakuwapo thamani ya fedha katika ununuzi wa umma na kuwapo ukuzaji uwajibikaji wa kifedha katika sekta ya umma," alisema.

Kimaro alisema taasisi yao imeandaa mada mbalimbali zitakazowasilishwa na watoa mada mahiri wa ndani na nje ya nchi.

Alitoa wito kwa wadau mbalimbali wakiwamo maofisa masuuli wa taasisi za serikali pamoja na wataalamu wa ununuzi wa umma, asasi za kiraia na wananchi kushiriki kwa wingi katika mkutano huo, unaotarajiwa kuwa na washiriki 300 (baadhi yao watashiriki kwa njia ya mtandao).

"Makundi haya hawapaswi kukosa fursa hii; wenye fani za ununuzi, uhasibu, uchumi, sheria, utabibu, waandishi wa habari, makandarasi na maofisa maendeleo ya jamii.

"Mkutano huu ni muhimu sana kwao kwa kuwa mada zitakazojadiliwa zinahusu moja kwa moja utendaji wa kazi zao," alisema Kimaro na kusisitiza kuwa washiriki ni sharti wajisajili kabla ya Julai 31 mwaka huu kupitia tovuti rasmi ya taasisi hiyo.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

**UZINDUZI WA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MKOA WA KIGOMA.**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uzinduzi wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza utafanyika Mkoa wa Kigoma tarehe 01 Julai, 2024. Mgeni Rasmi katika uzinduzi huo atakuwa Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (MB). Mara baada ya uzinduzi, zoezi la uboreshaji wa Daftari litaendelea Mkoani Kigoma hadi tarehe 07 Julai, 2024.

**Uboreshaji utahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuwani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo wataenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

Limetolewa leo tarehe 01/06/2024 na:

Kailima, R. K.
MKURUGENZI WA UCHAGUZI


## Nchi 8 zakutana kutatua changamoto watoto wanaolelewa nje ya familia zao

**Na Christina Mwakangale**

NCHI nane kutoka barani Afrika, ikiwamo Tanzania zimekutana jijini Dar es Salaam, kubadilishana uzoefu na mbinu za kukabiliana na changamoto kwa watoto waliolelewa nje ya familia zao kibaolojia.

Mratibu wa Vijana Taifa kutoka Vijiji vya Watoto SOS nchini, Samson Anthony, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye mkutano uliozikutanisha nchi hizo.

Alisema watoto wanaolelewa na kukulia kwenye makao kama vile vijiji hivyo, hukumbana na changamoto kwa kushindwa kuendana na mazingira kwenye jamii, siku chache baada kutoka maeneo ya malezi.

"Mara nyingi wanapotoka huku kwetu tulikowalea (vijiji/makao) ambako si katika familia za kibaolojia au kiasili, watoto huwa wanarudi tena kwetu kutaka msaada kwenye shirika.

"Sasa tulipobaini hilo, tumekutana ili kuja na mikakati kuwasaidia vijana pindi wanapotoka kwetu, wawe sawia na jamii, kuanzia kwenye familia na jamii kwa ujumla. Lengo la taasisi ni kuanzisha mtandao utakaokusanya vijana waliolelewa kwetu, tujue wako wapi, wanafanya nini," alisema Samson.

Alisema washiriki hao kutoka nchi hizo wanatoka katika SOS nchini mwao, watakuja na mbinu ikiwamo kuwaunganisha vijana waliowalea, kuwapa fursa za kiuchumi, kutokana na wengi wao kuwa ni wahitimu wa ngazi tofauti ya elimu kama chuo kikuu.

"Zimbabwe wamefanikiwa wana mtandao wenye nguvu na wanaweza kusukuma ajenda zao katika serikali kuleta mabadiliko kwa vijana. Tanzania na sisi mwaka jana, tuliunda mtandao, si wa SOS pekee bali na wengine waliolea vijana makao mengine, kufahamu kitu kipi cha kuwaunga mkono," alisema.

Alizitaja nchi zinazokutana kwa siku tano nchini kuwa ni Zimbabwe, Kenya, Rwanda, Zambia, Ghana, Afrika Kusini, Somalia na Tanzania.

Ofisa Uwezeshaji Vijana kutoka SOS Zanzibar, Eveline Baruti, alisema watoto wanaolelewa kwenye vituo kati ya changamoto zinazowakumba ni kushindwa kuchangamana na jamii.

"Tumewekeza katika ujasiriamali, makuzi na vipaji, hasa mafunzo stadi za kazi, ili wajiajiri. Zaidi tumefungua vituo vya Tehama na vijana wengi wananufaika, tunashirikiana na Baraza la Vijana Zanzibar," alisema Eveline.

Alisema watoto 57 wameunganishwa na familia zao, baada ya kuwalea huku mradi wa kuimarisha familia unaotekelezwa Unguja na Pemba, umewafikia zaidi ya watoto 5,000 pamoja na familia zipatazo 3,000 kuwawezesha kiuchumi.

# LHRC, THRDC wataka bajeti kuwalinda mwenye ualbino

Na Christina Mwakangale

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) pamoja na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC) wamelaani tukio la mauaji ya mtoto Asimwe Novath, wakishauri Bunge liitake serikali itenge bajeti ya ulinzi wa watu wenye ualbino.

Watetezi hao waliyasema hayo jana wakati wa mkutano na waandishi wa habari, mkoani Dar es Salaam, wakilaani kitendo cha utekwaji na mauaji yaliyotendwa dhidi ya mtoto huyo, huku mwili wake ukiopolewa siku 19 baadaye katika karavati baada kuchukuliwa kwa nguvu kutoka kwa mama yake.

Meneja Mipango wa THRDC, Remmy Lema, alisema wito wao kwa serikali ni Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu), kuweka mikakati kama vile kutambua watu wote wenye ualbino nchini kwa lengo la kukuza ustawi wao.

"Jeshi la Polisi lifanye uchunguzi wa kina juu ya tukio hili na kuhakikisha kuwa wahusika wote, ikiwamo walioratibu utekelezaj, uuaji na watumiaji viungo vya watu hao wanakamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria haraka," alisema Lema.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji LHRC, Fulgence Massawe, alitaka jamii iachane na imani potofu kuhusu matumizi ya viungo wenye ualbino kwa kuhusisha na kujipatia utajiri au shughuli za kisiasa.

Mtoto huyo (2), mkazi wa Kijiji cha Bulamuala, Kitongoji cha Mbale, Kata ya Kamachumu wilayani Muleba, mkoani Kagera, aliibwa na watu wasiojulikana Mei 30 mwaka huu baada kumvamia na kumkaba mama yake mzazi.

Siku 19 baadaye, mwili wake ulikutwa umetelekezwa katika karavati lenye maji barabarani eneo la Makongora, Kijiji cha Malelel, kwa mujibu wa Katibu Tawala Wilaya ya Muleba, Benjamin Mwkasege.

# Mgambo wanusurika kuuawa na wafugaji

Na Gideon Mwakanosya, NAMTUMBO

ASKARI watano wa Jeshi la Akiba (Mgambo) wa Kijiji cha Njomlole, wilayani Namtumbo, mkoani Ruvuma, wamenusurika kifo baada ya jamii ya wafugaji kutaka kuwashambulia kwa kutumia silaha za jadi wakati wakiondoa mifugo katika eneo lililotengwa kwa ajili ya kilimo.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Njomlole, Joseph Tembo alisema jana kuwa mgambo hao waliotumwa na ofisi yake kwenda kukamata mifugo iliyoingizwa katika skimu ya umwagiliaji kijijini huko walinusirika kuuawa na wafugaji waliokuwa na mikuki, mapanga, marungu na mishale.

Tembo alisema ofisi yake ilipewa taarifa na viongozi wa skimu ya umwagiliaji kuwa mazao yaliyoko katika skimu hiyo yanaliwa na mifugo iliyoingizwa na wafugaji.

Baada ya kupata taarifa hiyo na kuombwa kusaidia kukamata mifugo hiyo, Tembo alisema ofisi yake ilituma mgambo watano kufika eneo la kibanio walikokuta watoto wa jamii ya wafugaji wakilisha mifugo katika skimu ya umwagiliaji.

Tembo alidai mgambo hao walifanikiwa kukamata mifugo hiyo na kuanza kuondoka nayo. Watoto wa jamii ya wafugaji walikimbilia kwenye makazi yao kutoa taarifa.

Ni taarifa ambazo Tembo alisema zilisababisha vijana wa jamii hiyo, wakiwa na marungu, mapanga, mikuki na mishale, kuwakimbilia mgambo waliokuwa wakiswaga mifugo kwenda ofisini, wakitaka kuwadhuru.

Alisema kuwa mgambo hao baada ya kuona wanafuatwa na kundi kubwa la vijana, waliamua kuiacha mifugo na kukimbia, lakini baadhi yao walizingirwa kwa mbele na vijana hao wenye silaha za jadi.

Tembo alisema waliwaona mgambo wakitokea porini wakiwa wanahema na ndipo walipoeleza kilichotokea na hatari ambayo ilikuwa mbioni kuwatokea kama wangeendelea kuswaga mifugo.

Katibu wa Kamati ya Ulinzi wa Kijiji cha Njomlole, Edwin Mpepo alisema kuwa kama mgambo wa kijiji wangeng'ang'ania kuswaga ile mifugo, wangeshuhudia mauaji.

Mpepo alisema walipokea simu kutoka kwa mkulima, aliyemtaja kwa jina la Chrisant Ngailo, anayelima kwenye skimu ya umwagiliaji pamoja na mwenyekiti wa skimu ya umwagiliaji kulalamikia mifugo kuchungwa katika mashamba ya wakulima.

Mkulima Ngailo aliyeshuhudia tukio hilo akiwa kwenye skimu ya umwagiliaji, alisema aliona vijana wa jamii ya kifugaji wakiwa na silaha za jadi, ikampa ishara ya mapambano.

Alisema aliingiwa na hofu na kuamua kutoa taarifa kwa uongozi baada ya kuona vijana wa kifugaji wakikimbia kuwafuata mgambo waliokuwa wamekamata mifugo yao.

Winfridi Ngonyani, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Njomlole, alisema ameshatoa taarifa katika mamlaka za juu yake kuhusu kinachoendelea katika skimu hiyo.

Pia alithibitisha kuwa na taarifa za tukio hilo la mgambo kukimbizwa na wafugaji pamoja na kundi hilo kulishia mifugo katika skimu ya umwagiliaji mara kwa mara .

Alisema timu ya kata itakayoongozwa na Ofisa Mtendaji wa Kata, Ofisa Kilimo wa Kata na mgambo wa kata watatembelea maeneo hayo ili kuona namna ya kuwadhibiti wafugaji hao kutoendelea kuingiza mifugo katika skimu hiyo ya umwagiliaji.

Kijiji cha Njomlole kiko Kata ya Ligera, wilayani Namtumbo. Kimejengewa skimu ya umwagiliaji na serikali lakini skimu hiyo inakabiliwa na changamoto ya wafugaji wanaoigeuza kuwa eneo la malisho ya mifugo yao na kukwamisha malengo tarajiwa ya serikali ya kuwafanya wakulima kulima kisasa.





KWA USALAMA WA TANZANIA IJAYO

Miaka 5 ya Benkibima (Bancassurance), Ujenzi wa Sekta Inayoshamiri na Kupanua Upatikanaji wa Huduma za Bima Nchini

Sekta ya bima nchini inakua kwa kasi kubwa. Katika kuelezea mafanikio hayo Kampuni ya The Guardian Limited (TGL), itachapisha matoleo maalum katika magazeti yake ya **The Guardian** na **Nipashe** mwezi ujao yatakayojikita kuangalia upatikanaji huduma za bima zenye matokeo chanya kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Matoleo hayo yatajikita zaidi kuelezea:

- **Mafanikio ya Benkibima kwa Kipindi cha Miaka Mitano**
- **Jitihada za Kitaifa Kupanua Upatikanaji wa Huduma za Bima**
- **Mwelekeo wa Sekta ya Bima katika Serikali ya Awamu ya Sita**

Mradi huu wa ujumuishi wa huduma za kifedha ni jukwaa linalotoa fursa ya kipekee kwa watoa huduma za bima na wadau wengine kuonesha jinsi wanavyochangia ongezeko la upatikanaji huduma za bima na mapokeo yake nchini.

Usikose kutumia nafasi hii adimu kunadi taasisi yako na suluhisho bunifu dhidi ya majanga.

**Ili kupata maelezo zaidi ya jinsi ya kushiriki:**
**Wasiliana nasi kwa simu: 0714 791747, 0763214317, 0753 01427**
**Barua Pepe: advertise@guardian.co.tz**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uwekezaji majengo ya ubalozi nje utapunguza gharama

**UZINDUZI** wa majengo pacha ya ubalozi nchini Kenya yatakayotumika kama Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania umeeleza kuwa ni kitega uchumi kwa ajili ya kuongeza fedha za kigeni nchini.

Ofisi nyingi za balozi za Tanzania nchi za nje ni za kupangisha ambazo pia zinatengewa bajeti ili ziweze kujiendesha.

Kwa sasa imeelezwa kuwa Tanzania inatumia Sh. bilioni 29 kwa mwaka kulipia kodi kwa ajili ya balozi na makazi ya watumishi wake wanaofanya kazi nje ya nchi.

Kwa hiyo kwa ujenzi huo wa majengo pacha ni mkakati wa Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kutumia viwanja na majengo yake kuongeza mapato ya nchi.

Kwa mujibu wa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, majengo hayo ambayo ujenzi wake utagharamiwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa NSSF, yataipa Tanzania fursa ya kutumia majengo hayo kupangisha kwa makazi na ofisi ili kupata fedha.

Eneo litakalojengwa majengo hayo limitolewa bure na Serikali ya Kenya ikiwa ni kujibu ukarimu wa namna hiyo uliofanywa na Tanzania kwa kuipa Kenya bure eneo iliyojenga ofisi za ubalozi wake, Oysterbay, jijini Dar es Salaam.

Ushirikiano wa nchi hizi mbili ni wa muda mrefu kuanzia kwa watu wenyewe, kibiashara na kidiplomasia.

Eneo ambalo Tanzania imepewa kujenga ubalozi wake ni mojawapo ya maeneo ya kimkakati jijini Nairobi, kukiwa na ofisi nyingi za serikali.

Kwa mujibu wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu), Deo Ndejembi, uamuzi wa kujenga majengo hayo ulizingatia upembuzi yakinifu uliofanywa na wataalamu na kuona namna mradi utakavyoingiza mapato kwa serikali.

NSSF ina Kamati ya Uwekezaji ambayo kwa kushirikiana na Bodi ya Wakurugenzi na wataalamu wa masuala ya uwekezaji waliutazama mradi huo na kuona utakuwa na faida kwa Tanzania. Kwa sasa, mwelekeo ni kutazama miradi yenye faida na maslahi kwa taifa.

Miradi kama hii ya majengo ni uwekezaji mzuri na kwa NSSF, itawasaidia kutunisha mfuko wake ili wastaafu wafaidike na michango yao kwa kupata pensheni kwa wakati.

Kuwekeza kwenye miradi inayoleta faida inaleta matumaini hata kwa wafanyakazi wanaochangia kwenye mifuko ya jamii kwa kuelewa kuwa fedha zao zinakwenda kufanya uzalishaji.

Wakati uzinduzi wa majengo hayo ukifanyika, Waziri Mkuu na Waziri wa Mambo ya Nje wa Kenya, Musalia Mudavadi, ameipongeza hatua ya Tanzania kujenga jengo hilo akisema litakuwa mojawapo ya alama za kudumu za uhusiano wa kirafiki baina ya nchi hizo mbili.

Amesifia ubunifu wa majengo pacha kwa sababu utakuwa kielelezo na kumbukumbu kwamba Tanzania na Kenya ni pacha kwenye uhusiano.

Kwa ubunifu huo pia serikali ya Kenya imejifunza kitu kuhusu namna ya kutumia fedha za taasisi kama NSSF kwa kufanya uwekezaji ili zizalishe.

Tanzania ina jumla ya majengo 109 na viwanja 11 duniani. Pia ina jumla ya balozi 45 na Konseli Kuu tano duniani na kwa mujibu wa mkakati mpya uliopitishwa na Wizara ya Mambo ya Nje hivi karibuni, lengo la serikali ni kutaka kuona inatumia mali zake hizo kuingizia nchi mapato.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Tuntule Swebe

# Aina hii ya uzembe wetu katika taka, tujue tunakaribisha maradhi wenyewe

**NI** jambo la kawaida sana kwa jamii inayotuzunguka kutupa taka sehemu ambazo wala sio sahihi mathalani kwenye mitaro inayotumika kusafirisha maji. Niseme, jambo hili haliko sawa.

Watu wengi wanapokuwa barabarani au majumbani mwao, imekuwa ni kawaida yao kutupa taka pasikofaa, wakikwepa gharama za kulipia taka, hivyo, inawalazimu watupe kwenye mitaro jirani.

Kuna baadhi yao, wanaona shida kutembea na taka aliyoizalisha, kama baada ya kunywa soda, kula matunda, kunywa maji. Hivyo, anaona ni bora atupe kwenye mtaro, wakisahau kuwa wakati mwingine, taka zina mbadala wa kumnufaisha, ikitumika kwa busara.

Kwa taka zinazotupwa kwenye mitaro majumbani, watu wanaokaa karibu na wanakuwa hatarini na maradhi kama ya tumbo na kipindupindu.

Uchafu unaotupwa, unachangia maji kukwama na ndio unakuwa mwanzo wa simulizi za mlipuko wa maradhi.

Mbu wakienea, tayari wanajamii mnakuwa jirani na maradhi kama matende na malaria, hivyo watu wanaoishi jirani, wanabaki kuishi kwa hofu na mtu akigua, shughuli za maendeleo husita au kusuasua, kila kona na hata kuna baadhi wanaweza kupoteza uhai.

Tusisahau pia, kunapokuwapo mvua kubwa, kunaweza kuwapo mafuriko. Je, tumewahi kujiuliza na sisi wenyewe ni wapi tunapokosea?

Kuna baadhi ya sehemu zinazotiririsha maji zinahitaji marekebisho. Kama, wananchi tutaendekeza utupaji taka mitaroni, inachangia maji yasiende na mvua inapokuwa kubwa, maji hujaa mitaroni au ikafurika, ikihamia kwenye makazi ya watu.

Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, sasa inatambua ongezeko la aina tofauti za taka ngumu, zikiwamo taka za majumbani, viwandani na taka za hospitalini zinatupwa maeneo mbalimbali, hivyo kuweza kusababisha uchafuzi wa mazingira (hewa, maji na ardhi).

Dar es Salaam linakadiriwa kuzalisha zaidi ya tani 4,600 za taka kwa siku. Kati ya hizo, asilimia 45 hadi 50 tu zinazopokelewa katika dampo, sawa na tani 2,070 hadi 2,300, kwenye maeneo ya wazi, mitaro ya maji, barabara na makazi.

Usafi wa Dar es Salaam, husani udhibiti taka ngumu, ni tatizo la muda mrefu na lenye changamoto nyingi.

Tabia iliyozoeleka miongoni mwa jamii kutupa ovyo taka katika maeneo yasiyostahili, imechangia uchafu wa Dar es Salaam.

Kuzagaa taka kunaweza kuwa kichocheo cha milipuko ya magonjwa, kama vile kipindupindu ya kuhara na kutapika.

Uchafu wa Dar es Salaam, unachangiwa pia na elimu ndogo kuhusu usafi wa mazingira na kutotii sheria zilizopo kwa upande wa wananchi na usimamizi hafifu wa sheria za usafi wa mazingira.

Ili kupunguza uchafuzi wa mazingira, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, imeandaa sera ya kurejeleza taka ngumu, itakayokuwa msingi kwa taasisi za nchini kutambua na kurasimisha sekta ya urejelezaji taka, ambao awali iliendeshwa na taasisi binafsi, pia vikundi visivyokuwa rasmi.

Katika kuhakikisha hilo linafanyika, Halmashauri ya Jiji la Dar Es Salaam inalenga kufanya mambo kadhaa:

Kwanza, inabuni miradi ndani ya jiji itakayohusisha wadau kurejeleza taka, pamoja na kupatikana masoko ya uhakika kwa bidhaa zitakazozalishwa kupitia uchakataji huo.

Ingependeza, jamii ikahamasishwa umuhimu wa kurejeleza taka, ikishirikiana na halmashauri za manispaa kuhakikisha utenganishaji taka ufanyike kuanzia ngazi za uzalishaji (sorting at source).

Lingine linatajwa ni kuwatambua na kuwaunganisha wadau wanaojihusisha na teknolojia za urejelezaji taka ndani ya Dar es Salaam, kukitengwa maeneo.

Hapo ndani yake kuna suala la kuwezesha wananchi wa maisha ya chini, wakiwamo vijana na wanawake, wakashiriki katika ubunifu na utumiaji teknolojia za urejelezaji taka, hatimaye kufikia suala la usafi.

Urejelezaji huo wa taka una faida nyingi kama vile; kuongeza thamani ya taka na kipato katika jamii, kupunguza marundo ya taka katika mitaa na maeneo ya jamii, kupunguza gharama za uendeshaji wa dampo, kupunguza gharama za udhibiti taka.

Hivyo, kama wanajamii kwa pamoja tukemee utupaji taka kwenye mitaro, kwani mvua ikinyesha, maji yanasimama na kukosa mwelekeo.

# Serikali yataka chombo ithibati sekta ya afya

**Na Joseph Mwendapole**

WIZARA ya Afya imesema kuna umuhimu wa kuwa na chombo huru kitakachokuwa na jukumu la kutoa ithibati na kudhibiti ubora wa huduma za afya zinazotolewa nchini ili kukidhi viwango vya kitaifa na kimataifa na kukuza utalii tiba nchini.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. Grace Magembe, wakati wa ufunguzi wa kongamano la siku moja la wataalamu wa afya wa Tanzania na Uingereza linaloendelea jijini Dar es Salaam.

"Nawapongeza sana Taasisi ya Watanzania wanaoishi nchini Uingereza (Diaspora) ambao wanashirikiana na taasisi zetu za afya hapa nchini katika mafunzo, utafiti na ubunifu ikiwamo matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika tiba (TEHAMA)," alisema.

Aidha, alisema ushirikiano huo ni muhimu kwa kuwa unasaidia kupeleka huduma za kibingwa na bobezi kuwa bora na hivyo kuwezesha nchi kuwa kitovu cha tiba utalii kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati.

"Niwaombe sana wataalamu hawa pamoja na maeneo hayo ambayo tumeanza kushirikiana, tushirikiane nao pia katika kuandaa miongozo na hatimaye chombo ambacho kitakuwa na jukumu la kutoa ithibati ya utoaji wa huduma za afya kwa lengo la kudhibiti ubora wa huduma za afya nchini kama wanavyofanya nchini Uingereza," alisema.

"Nimesikiliza mada ya mtaalamu kutoka Uingereza ambaye ameeleza namna mfumo wa ithibati na udhibiti ubora wa huduma za tiba unavyofanyika na namna wanavyochukua hatua stahiki huko nikaona na sisi tunaweza kufanya hivyo na ikatusaidia," alisema Maghembe.

Alisema tayari zipo taasisi na mabaraza ambayo yanafanya kazi hiyo, lakini bado kuna maboresho yanayotakiwa kufanyika kwa lengo la kujiweka katika nafasi ya juu zaidi kwa kufuata vigezo vya kitaifa na kimataifa.

"Tunahitaji kuwa na chombo huru kitakachotuambia hapa tunafanya vizuri na hapa hatufanyi vizuri, kwa lengo la kuboresha huduma zetu zaidi na zaidi," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa ya jijini Dodoma, Prof. Abel Makubi, alisema kongamano hilo la kitaaluma lina lengo la kubadilishana uzoefu katika masuala mbalimbali ya matibabu.

Naye Mwekahazina wa Jumuiya ya Watanzania wanaoishi Uingereza wanaojihusisha na masula ya afya (TUHEDA), Prof. Gideon Mlawa, alisema ushirikiano baina ya jumuiya hiyo na Tanzania utajikita zaidi katika kubadilishana wataalamu, mafunzo na utafiti kwa lengo la kuboresha huduma.

"Katika ushirikiano huu sisi Watanzania tunaoishi Uingereza tunarudisha nyumbani kile tulichokipata ikiwa ni pamoja na utaalamu, lakini tutarudi kujenga viwanda vya dawa na vifaa tiba ili kuinua sekta ya afya nchini," alisema.

Wataalamu wa afya kutoka Hospitali ya Taifa, Rufani Kanda na mikoa nchini wamekutana na wenzao kutoka Hospitali Queen-Elizabeth ya Uingereza chini ya uratibu wa TUHEDA ili kujadiliana mbinu mbalimbali za uboreshaji wa tiba na huduma za afya nchini.



Wananchi wakipishana na magari, baada ya eneo la waenda kwa miguu kujaa maji kando ya Barabara ya Bagamoyo, eneo la Mwenge, kutokana na mvua kubwa iliyonyesha Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Tathmini: Zaidi ekari 75,000 za mazao zimeathiriwa mafuriko

**Na Paul Mabeja,**
DODOMA

SERIKALI imesema kuwa tathmini ya awali inaonyesha kuwa takribani ekari 75,594 za mazao nchini ziliharibiwa katika mikoa iliyoathirika na mafuriko, wakati wa mvua ya El-nino, mwaka huu.

Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde, alisema hayo jana bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum Sylvia Sigula, aliyetaka kujua serikali inawasaidia vipi wakulima ambao mazao yao yameharibiwa na mafuriko.

Akijibu swali hilo Silinde alisema tathmini ya awali inaonesha ekari 75,594 za mazao ziliharibiwa katika mikoa iliyoathirika na mafuriko.

Alisema ili kuwezesha wakulima katika maeneo hayo kuendelea na shughuli za kilimo, serikali kwa kushirikiana na wadau imetoa msaada wa pembejeo ikijumuisha tani 70 za mbolea, tani 5.6 za mbegu bora za mahindi, maharage, ngano na alizeti.

Alisema maandalizi ya kusambaza mbegu za mahindi tani 748.4 na mpunga tani 449 yanaendelea kwa ajili ya Halmashauri za Wilaya ya Kibiti na Rufiji kwa msimu wa 2024/2025.

Alisema serikali itaendelea kufuatilia hali ya uzalishaji wa mazao ya kilimo na usalama wa chakula katika maeneo yote na kuchukua hatua stahiki.

**Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde, alisema hayo jana bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum Sylvia Sigula, aliyetaka kujua serikali inawasaidia vipi wakulima ambao mazao yao yameharibiwa na mafuriko.**

"Serikali inapenda kuwapa pole waathirika wote wa mafuriko yaliyotokana na mvua ya El-nino iliyonyesha katika msimu wa mwaka 2023/2024 katika maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwamo mikoa ya Manyara, Morogoro, Pwani na Mbeya," alisema.

Alisema kutokana na athari hizo, serikali imechukua hatua za haraka na za muda mfupi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kusaidia waathirika kwa kuwapatia msaada wa kibinadamu ikiwa ni pamoja na chakula.

"Hadi kufikia mwezi Aprili, 2024 serikali ilisambaza jumla ya tani 1,043.34 za mahindi ya chakula katika maeneo hayo," alisema Silinde.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Doyo ajitosa kugombea uenyekiti ADC

**Na Elizabeth Zaya**

KATIBU Mkuu wa Chama cha Alliance for Democracy Change (ADC), Doyo Hassan Doyo, amejitosa kutia nia ya kugombea uenyekiti wa chama hicho kumrithi Hamad Rashid Mohamed, ambaye amemaliza muda wake.

Hamad na Doyo ni miongoni mwa waliokihama Chama cha Wananchi(CUF), na kuanzisha Chama cha ADC baada ya kuibuka kwa mgogoro.

Kabla ya kushika nafasi hiyo ya uenyekiti, Hamad alikuwa anakilea na mwanzoni mwa mwaka 2016 baada ya kufanyika uchaguzi alichaguliwa rasmi kukiongoza katika nafasi hiyo huku Doyo akichaguliwa kuwa Katibu Mkuu na mpaka sasa wawili hao wametumikia katika nafasi zao kwa miaka 10.

Tayari Hamad Rashid, alishatangaza kung'atuka katika nafasi hiyo ili kupisha kuchaguliwa mrithi wake kama Katiba wa chama hicho inavyotaka katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Juni 29, mwaka huu.

Jana Doyo alirejesha fomu ya kuwania nafasi hiyo mbele ya Kamati ya uchaguzi ya chama hicho.

Mbali na Doyo, mwingine aliyerejesha fomu hiyo jana ni mgombea wa nafasi ya Makamu Mwenyekiti Bara, Scola Kahana, ambaye aligombea ubunge Jimbo la Kibaha Mjini mwaka 2020 kupitia ADC.

Akipokea fomu hizo, Katibu wa Kamati ya Uchaguzi ADC, Innocent Siriwa, aliwataka wagombea wote kufuata taratibu na kanuni za uchaguzi ili kulinda amani.

"Hatua hii inaonyesha ukomavu wa kisiasa hasa pale ambapo viongozi wanapokubali kuachia madaraka kwa mujibu wa kanuni na sheria za katiba bila kulazimishwa.

"Natoa wito kwa wagombea kuzingatia taratibu zote zilizopo ili itakapofika tarehe 29, mwaka huu twende kwenye uchaguzi ambao tuna imani utakuwa huru na haki," alisema Siriwa.

Akizungumza wakati akirejesha fomu hiyo, Doyo alisema ameona anatosha kugombea nafasi hiyo na endapo atafanikiwa atapambana ili kuendelea kukiimarisha chama hicho kufikia viwango vya juu kwa kuzingatia kulinda amani na utulivu wa nchi.

"Kutokana na uzoefu wa miaka 10 nilioupata kutoka kwa mwenyekiti aliyemaliza muda wake naahidi kuyaendeleza mazuri yote hususan kuilinda katiba ya chama chetu.

Doyo alisema endapo atafanikiwa kushinda nafasi hiyo atakisaidia chama kusukuma ajenda za upatikanaji wa ajira, elimu bora, na kupata wabunge wawakilishi watakaowakilisha wananchi katika changamoto zao bungeni.




Mgombea nafasi ya uenyekiti Taifa wa Chama cha Alliance for Democratic Change-ADC, Doyo Hassan (kushoto) na mgombea nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Scola Deonatus (kulia), wakiwa katika maandamano wakati wa kurudisha fomu makao makuu ya chama hicho, Buguruni jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

KCBL KILIMANJARO CO-OPERATIVE BANK LIMITED
Together, Transforming Lives

**TANGAZO**

TUNAPENDA KUWAARIFU WENYEVITI NA WAJUMBE WA BODI WA VYAMA, MAKAMPUNI/TAASISI NA WANAHISA WOTE BINAFSI, KUWA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA SABA (27) WA MWAKA WA WANAHISA WA BENKI YA USHIRIKA YA KILIMANJARO (KCBL), UTAFANYIKA SIKU YA IJUMAA, TAREHE 26 JULAI, 2024 KWENYE **UKUMBI MABELE HALL (MABEYO COMPLEX), JIJINI DODOMA** KUANZIA SAA TATU (3:00) ASUBUHI.

TUNAPENDA KUWAKUMBUSHA KUWA KILA CHAMA/TAASISI/KAMPUNI ITUME **MJUMBE MMOJA TU**, NA MWANAHISA BINAFSI ANAYO NAFASI YA KUHUDHURIA BINAFSI AU KUWAKILISHWA KWA MUJIBU WA MASHARTI YA BENKI.

KARIBUNI SANA.

Godfrey J. Ng'urah,
**KATIBU-BODI YA WAKURUGENZI**

Tarehe: 19/06/2024

# Watatu wahukumiwa kunyongwa hadi kufa

**Na Halima Ikunji,**
TABORA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Tabora, imewahukumu kunyongwa hadi kufa watu watatu waliokuwa wanakabiliwa na kesi mbili tofauti baada ya kuwatia hatiani kwa kutenda makosa ya mauaji, huku wengine wawili wakipewa adhabu ya kifungo nje ya gereza miezi 12.

Adhabu hizo zimetolewa na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Mkoa wa Tabora, Jovity Katto, aliyekasimiwa mamlaka ya ziada kusikiliza mashauri ya Mahakama Kuu.

Waliohukumiwa kunyongwa hadi kufa ni pamoja na Seleman Haruna, ambaye alisababisha kifo cha Nyamizi Ally, mwanafunzi wa darasa la nne ambaye alikuwa ni mtoto wa mkewe, baada ya kumpa kinywaji chenye sumu ya kuulia wadudu waharibifu.

Akitoa adhabu ya kesi hiyo hakimu Katto, alisema Mahakama imeridhika pasiposhaka na ushahidi wa upande wa mashtaka, kwamba ulitenda kosa hilo kwa makusudi hivyo haiwezi kumwonea huruma, hivyo atanyongwa hadi kufa.

Awali upande wa Jamhuri, ukiongozwa na wakili Nurdin Mmari, ulidai kuwa mshtakiwa Haruna alitenda kosa hilo Aprili 28, 2019 huko Kaliua kwa kumpa juisi yenye sumu mtoto huyo.

Wengine waliohukumiwa kunyongwa hadi kufa ni Pesa Making'ombe na Juma Pana ambao kwa pamoja wakiwa na wenzao ambao bado hawajakamatwa walimuua, Charles Mbojo, kwa kumkatakata sehemu mbalimbali za mwili wake kwa mapanga.

Washtakiwa walitenda kosa hilo, Julai 7, 2020 usiku, huko Ulyankulu baada ya kuvamia nyumbani kwa marehemu na kuvunja mlango na kisha kutoweka kijijini hapo na kukamatwa baada ya miezi 11.

Shahidi katika kesi hiyo Kuligwa Masiligani, ambaye ni mke wa marehemu, aliiambia mahakama kuwa aliwatambua washtakiwa kupitia mwanga wa taa ya sola, baada ya kuingia ndani walimkuta yeye na kumfungia katika chumba walichokuwa wakitumia kama jiko.

Waliopewa adhabu ya kifungo cha nje ya gereza miezi 12 ni Lucia Maria na Joseph Kapingu, aliyekuwa akikabiliwa na shtaka la kujaribu kuua.



# Aliyesababisha ajali ya Katibu Tawala Kilimanjaro asakwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MAKACHERO wa Jeshi la Polisi mkoani Kilimanjaro wanamsaka Godlisten Kileo, dereva wa lori la kusafirisha nishati safi ya gesi, aliyesababisha ajali iliyoua watu wawili, akiwamo Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro (RAS), Dk. Tixon Nzunda (56).

Kileo, aliyekuwa akiendesha lori aina ya scania, lenye namba za usajili T 655 ABY alitoroka Juni 18 mwaka huu, baada ya kusababisha ajali hiyo katika eneo la Mjohoroni-Palestina, Kata ya KIA, Wilaya ya Hai, wakati kiongozi huyo akiwahi msafara wa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na ujumbe wake.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi, mkoani humo, Kamishna Mwandamizi Msaidizi (SACP), Simon Maigwa, licha ya chanzo cha ajali hiyo kuendelea kuchunguzwa, polisi imeanzisha msako wa kutamfuta dereva huyo aliyetoroka baada ya ajali.

Alisema chanzo cha ajali ni uzembe wa dereva wa gari namba T 655 ABY aina ya scania, mali ya kampuni ya Orange Gas, kushindwa kulimudu gari lake na kwenda kugonga gari lingine.

Ajali hiyo iliyohusisha lori aina ya scania na toyota landcruiser V8 (GXR), lenye namba za usajili STM 7476, ilisababisha vifo viwili, cha Dk. Nzunda na dereva wake, Alphonce Edson (54).

Marehemu Dk. Nzunda, alikuwa akielekea Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), kumpokea Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na ujumbe wake.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, akitangaza taarifa za kifo cha Dk. Nzunda, alisema Dk. Nzunda na dereva wake walipoteza maisha, majira ya saa 8:30 mchana katika eneo la Mjohoroni (Palestina), Wilaya ya Hai.

Dk. Nzunda wakati wa uhai wake, aliteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Machi 16, 2023.

Vilevile, Februari 28, 2021, Hayati Dk. John Magufuli aliyekuwa Rais, alimteua Dk. Nzunda kuwa Naibu Katibu Mkuu-TAMISEMI.



Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mkoa wa Manyara, Mhandisi Walter Kirita (wa pili kulia), akitoa ufafanuzi kuhusu utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji wa Dambia – Haydom, wilayani Mbulu utakaogharimu Sh. bilioni 41 na kunufaisha vijiji 20, kwa wajumbe wa kamati ya siasa ya CCM ya mkoa huo, ilipotembelea mradi huo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Madawati ya jinsia 297 yaanzishwa vyuo vikuu, kati

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Felister Mdemu, amesema hadi kufikia sasa kuna madawati 297 pekee yaliyoanzishwa nchini kati ya 612 yanayotakiwa kuanzishwa katika Taasisi za Elimu ya Juu na Vyuo vya Kati Tanzania Bara.

Amesema pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau katika kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia, bado kuna viashiria na matukio hayo vinavyoendelea kuripotiwa kwenye vyuo vikuu, huku madhara yake yakiwa makubwa.

Alitoa takwimu hizo juzi wakati akizungumza katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), na wakuu wa vyuo na waratibu wa madawati ya jinsia katika taasisi za elimu ya juu na kati, Mdemu.

Alisema waathirika wa ukatili, hasa rushwa ya ngono, wamekuwa wakipata madhara mbalimbali, yakiwemo matatizo ya kisaikolojia, baadhi ya wanafunzi kushindwa kuendelea na masomo na maambukizi ya magonjwa kama Ukimwi.

Aidha, Naibu Katibu Mkuu huyo, alisema madhara mengine ni kuzalisha wahitimu wasiokuwa na sifa stahiki, ambao hawawezi kutoa matokeo tarajiwa.

Kutokana na hali hiyo, aliagiza wakuu wa vyuo vyote nchini kutenga bajeti ya shughuli za uendeshaji wa dawati, ili kuhakikisha kuwa madawati hayo yanafunguliwa na kuleta tija, kwa kuwa msaada katika jamii.

"Madawati haya ni nyenzo muhimu ya kuweka ulinzi na mfumo wa kushughulikia matukio ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia katika vyuo vikuu, ikiwemo rushwa ya ngono, kwani vitendo hivyo havikubaliki kwa kuwa madhara yake makubwa,"alisema Mdemu.

Mwaka 2021, wakati wa uzinduzi wa siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alielekeza vyuo vyote nchini kuanzisha madawati hayo.

Awali, Mkurugenzi Msaidizi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Irene Gondwe, alisema mafunzo kuhusu namna bora ya uanzishaji wa madawati hayo, yanalenga kujengeana uelewa.

Uanzishaji wa dawati la jinsia katika taasisi za elimu ya juu na elimu ya kati ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000), ambayo imefanyiwa mapitio; na sasa inaitwa Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2023.

Mkakati huo unachagizwa pia na Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA 2024/25-2829).

Kwa mujibu wa Godwe, jukumu hilo linahusisha uratibu na ufuatiliaji wa juhudi za kuzuia na kutokomeza vitendo vya ukatili na unyanyasaji kijinsia katika ngazi mbalimbali.

## Askofu awapa ujumbe watoto kuhusu mafanikio

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Elimu Pentecoste Tanzania (KEPT), Peter Konki, ameisihi jamii na hasa watoto wanaotoka katika familia masikini kutokubali kukatisha ndoto zao.

Badala yake amewataka kukubali changamoto na kutumia vipaji au talanta zao kusonga mbele kufikia maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Alitoa rai hiyo wakati akizungumza katika Shule ya Sekondari Singe ya Babati, kuhusu ulinzi na usalama wa watoto waliojitokeza kushiriki uzinduzi wa tamasha la kuibua vipaji kwa watoto 'kipaji changu maisha yangu', lililoandaliwa na shirika la Compassion International Tanzania.

"Wako watu wanakatisha wenzao tamaa kuhusu maisha. Hebu Watanzania tuache kuwakatisha tamaa wananchi kwa kuwaita masikini, hali inayosababisha washindwe kuchangia na kushiriki kikamilifu katika miradi na shughuli za maendeleo, hususani miradi ambayo ina ufadhili kidogo wa serikali na wahisani," alisema.

Akizungumzia mradi huo, Kaimu Meneja wa Ushirika Wenza wa Kanda ya Ngorongoro, inayoundwa na klasta 11 za Compassion Intenational, Erasto Malila, alisema ili kuwaondoa Watanzania katika hali hiyo, zaidi ya watoto na vijana 400 wanashiriki tamasha hilo.

Aidha, alisema vigezo vilivyotumika kuwapa nafasi ya kushiriki ni baada ya watoto 400 kuwahi kubainika wana vipaji kutoka kwenye makanisa yao.

Alisema mkakati walionao ni kuibua mahitaji halisi ya watoto na kuyaweka kwenye mpango wa kanisa, ambapo kutakuwepo na bajeti ya makanisa ili yaweze kuwasaidia watoto.

Malila alisema bajeti itakuwa inapitishwa na wawezeshaji na kufanya ufuatiliaji kila baada ya miezi mitatu na kila mwezi kutakuwepo na ukaguzi, hivyo hakuna ufujaji wa fedha za kuibua vipaji vya watoto.

Awali, Mwenyekiti wa Klasta ya Babati, Jonathan Mbesere, alisema washiriki wa tamasha hilo ni kuanzia miaka 15 hadi 22, ambapo tamasha lilianza Juni 17 na litaisha Juni 21 mwaka huu.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Babati, Lazaro Twange, alisema serikali ipo tayari kupokea vipaji vyao ila waheshimu jambo lililowakutanisha na kuheshimu kanuni na taratibu.







Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, akizungumza na wananchi waliofika kupima afya zao katika Kambi ya Madaktari Bingwa wa Rais Samia Suluhu Hassan, katika Hospitali ya Manispaa ya Shinyanga juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Ahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa kumuua mjomba

**Na Mwandishi Wetu,**
TABORA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Tabora, imemhukumu kunyongwa hadi kufa mkazi wa Wilaya ya Kaliua, Raphael Nestory pamoja na kutoa adhabu ya kifungo cha miaka minne hadi 10 jela washtakiwa wiwili, baada ya kukutwa na hatia ya kuua bila kukusudia.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu wa Mahakama ya Mkoa wa Tabora, Jovith Katto, aliyekasimishwa mamlaka ya ziada ya kusikiliza mashauri ya Mahakama Kuu, alisema Nestory, alishirikiana na wenzake kumuua mjomba wake, Elikana Lugaka, kisha kumfukia.

Katika shauri hilo, mahakama hiyo ilimwachilia huru mshtakiwa wa kwanza, Mwendapole Mayala baada ya kukosekana ushahidi wa kumtia hatiani.

Upande wa mashtaka katika kesi hiyo, ulieleza kuwa mshtakiwa (Nestory), akiwa na wenzake wawili ambao ni watoto wa marehemu Lugiko, walitenda kosa hilo Juni 4, 2020 kwa madai ya marehemu huyo alikataa kuwapatia urithi wa mali ikiwamo ng'ombe alizokuwa akimiliki.

Ulieleza kuwa watuhumiwa hao walipanga jinsi ya kumuua baba yao, walipotimiza adhima hiyo walimfukia ndani ya shimo, kisha kutokomea kusikojulikana.

Katika hatua nyingine, mahakama hiyo kwa kutumia Kifungu Namba 300 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, imebadilisha hati ya mashtaka na kumtia hatiani kwenda jela miaka minne kwa kosa dogo la kuua bila kukusudia, Twaha Shaban, aliyekuwa akikabiliwa na kesi ya mauaji.

Baada ya kusikiliza maelezo ya pande zote mbili, Hakimu Katto, alisema kwa kutumia mamlaka aliyopewa na kwa kutumia Kifungu Kidogo cha Kwanza Namba 300 anabadilisha shtaka la mauaji kuwa kosa dogo la kuua bila kukusudia.

Alisema kifungu hicho cha Sheria ya Makosa ya Jinai kinaeleza kuwa, wakati mtu anashtakiwa na kosa na maelezo yanathibitisha kwa kupunguza kosa na kuwa dogo, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa hilo dogo japokuwa hakushtakiwa na kosa hilo.

Twaha Shaban, alikuwa anashtakiwa kwa kosa la kumuua mke wa mtoto wake, kisha kumfukia ndani ya shimo, tukio ambalo linadaiwa kutokea Januari 4 mwaka 2023 katika Kijiji cha Malanga Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora.

Vilevile, mahakama hiyo imemhukumu, Juma Ramadhan kwenda jela miaka 10 baada ya kumkuta na hatia kwa kosa la kumuua mkewe bila kukusudia.


Lindi Jumbo
Limited

JOB VACANCY

IT COORDINATOR

**Location:** Matambarale, Ruangwa District, Tanzania.
**Closing Date:** 28 June 2024, 5:00PM (EAT)
**To apply and view more details visit:** https://jobportunities.net/jobs_search.aspx



**For assistance on the portal, please contact the Tara Nawa team at +264 (0) 64 402403, WhatsApp +264812294611 or +255 0616 – 007 201**
**Alternatively send an email via the recruitment portal's Contact Us page.**


# Mil.200/- kumaliza kero ya maji Magu

**Na Rose Jacob,**
MAGU

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda, amezindua mradi wa maji wa Sh.milioni 215 katika Kijiji cha Kabila wilayani Magu mkoani hapa.

Akizindua mradi huo uliofadhiliwa na Kampuni ya Bia Serengeti na shirika lisilo la kiserikali la African Community Advancement Initiative (AFRIcai), juzi

Mtanda alisema mradi huo utasaidia kuondoa adha ya upatikanaji wa maji iliyokuwapo kwa muda mrefu kwa wakazi zaidi ya 12,000 wa eneo hilo.

"Mashirika haya binafsi yamekuwa mstari wa mbele katika kukuza miradi ya maendeleo nchini ambayo inawezesha kuwapo kwa jamii iliyo na uzalishaji na afya bora kadhalika ushirikiano kati ya SBL na AFRIcai unathibitisha dhamira ya sekta binafsi kwa uwajibikaji wa kijamii na maendeleo endelevu," alisema Mtanda.

Aidha, alisema mradi huo unahusisha ufungaji wa pampu ya kuzamisha ndani ya kisima, ujenzi wa nyumba ya pampu, tangi la kuhifadhi maji, mtandao wa mabomba ya maji na vituo vipya vya maji 13 vyenye uwezo wa kutoa mita za ujazo 87,000 za maji kwa mwaka.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Obinna Anyalebechi, alisema mradi huo ambao unajulikana, kama 'maji kwa ajili ya uhai' ni miongoni mwa mikakati ambayo kampuni hiyo inaendesha katika mikoa ya Iringa, Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Mwanza, Singida, Mara, Tanga, Ruvuma, Dar es Salaam, Pwani na Dodoma ikiwa imewanufaisha zaidi ya watu milioni mbili kwa majisafi na salama.

Meneja wa Mawasiliano na Uendelevu wa SBL, Rispa Hatibu alisema: "Mradi wa kabila siyo tu kwamba utaboresha afya za wakazi wa eneo hilo bali utaongeza tija kiuchumi hususani kwa watoto wa kike na wanawake ambao hawatahitaji kutumia saa nyingi kutafuta majisafi na salama sehemu nyingine."

Mkurugenzi Mtendaji wa AFRIcai, Bonus Caesar, alisema sera zao zinajikita katika ustawi wa jamii katika maeneo ya maji, afya, elimu na uwezeshaji.

# RC atoa siku 21 walioahidi fedha ujenzi wa shule kutimiza

**Na Elizabeth Selemani,**
SENGEREMA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda amewataka wadau waliotoa ahadi za fedha katika harambee ya kuchangia ukamilishaji wa ujenzi wa Shule ya Msingi Pambalu, watimize ndani ya wiki tatu.

Alitoa agizo hilo wilayani Sengerema mkoani hapa wakati akizungumza na wananchi wa maeneo hayo.

Mtanda alisema madarasa yanatakiwa kukamilika lakini fedha hazijatolewa, hivyo kuwataka wadau waliotoa ahadi hizo wakamilishe ndani ya wiki tatu.

Aidha, alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Sengerema, Binuru Shekidele, kuhakikisha anawafuatilia waliotoa ahadi hizo, ikiwamo ofisi yake, ya DC (Mkuu wa Wilaya) na ya Mkuu wa Mkoa huo ndani ya siku 21 wawe wamaliza michango yao.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Binuru Shekidele, alisema amepokea agizo hilo, huku akiahidi kulitekeleza ndani ya muda uliopangwa.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Makoye Sengerema, alisema ofisi ya mwenyekiti iliahidi fedha za ujenzi wa madarasa ya shule tajwa hapo juu, hivyo itatekeleza haraka.

Akiongea kwa niaba ya wazazi wa Shule ya Msingi Pambalu, Fransisco Shilinde, alisema tangu mwaka 2022 walifanya harambee hiyo, lakini hadi leo hakuna mtu ambaye ameweza kutimiza ahadi, hivyo alimshukuru Mkuu wa Mkoa kwa kutoa maelekezo hayo.

ama
ALHAMISI JUNI 20, 2024
AFYA NA MAZINGIRA

Ukurasa 13



**BAADA NIPASHE KUANIKA...**
**Zahanati iliyokwama miaka 14, hatimaye inajengwa kwa kasi**




**KUKITHIRI SHIDA AFYA AKILI...**
**Bajeti tiba juu, Hospitali Mirembe yaboreshwa; kozi mpya zimeanza**

Ukurasa 12

# Awamu ya Sita ilivyopokea 'hodi' UVIKO 19, hadi hatua ya 'baibai'

## • Fedha za ugonjwa zilivyovusha maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kilio cha kuzuka maradhi ya Uviko 19 duniani mwaka mmoja kabla ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuingia madarakani, utata ulizingira wa ama kuwapo au kutokuwapo maradhi hayo nchini. Baadaye ikawa rasmi kwamba upo.

Lakini, kupita mwaka mmoja akiwa madarakani, Rais Dk. Samia, ambaye alishatumikia miezi kadhaa kupokea nafasi ya mtangulizi wake, marehemu, Dk. John Magufuli, akatoa ufafanuzi wa kuukabili.

Akaanza na wito kwa wananchi wote "kila mmoja kwa nafasi yake kulinda afya, kwani ulinzi huo unaanza na mtu mwenyewe."

Ni kauli yake akiwa Bungeni jijini Dodoma, katika hotuba yake wakati akielezea hali ya afya na hatua ambazoTanzania imezichukua kukabiliana na ugonjwa wa Korona 19.

Rais Dk. Samia akafafanua: "Ugonjwa huu umeathiri dunia nzima na mbaya zaidi ni kwamba janga hili linapungua na kurudi katika mifumo tofauti tofauti.

'Mpaka sasa bado hakujawa na dalili za kupatikana kwa tiba ya maradhi haya. Njia pekee iliyopo ni kujikinga na kuchukua hatua mbalimbali za tahadhari."

Akaendelea: "Hapa nchini tumekuwa tukifuata miongozo kadhaa ya kinga inayotolewa na wataalamu na kwa kutumia njia zetu za tiba asilia tumeweza kwa kiasi kikubwa kushusha kiwango cha maambukizi.

"Hapa nchini tumeamua kuunda Kamati ya Wataalamu ambao kwa kushirikiana na taasisi za Afya Duniani na zile za kikanda za EAC (Jumuiya ya Afrika Mashariki) na SADC, wataliangalia suala hili kwa undani, kufanya uchambuzi wa kina na kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua na jinsi ya kuendelea kupambana na maradhi hayo."

Hadi sasa hatua zilizochukuliwa ni mbinu za kimataifa zikiwamo watu kuchanjwa mara ya kwanza na sasa iko awamu ya pili, watu kuwa na uhakika wa kinga za miili yao.

Ufafanuzi wa kitaalamu wa mwanzo, ulijumuisha mhusika mkuu, Wizara ya Afya kupitia kwa Dk Leonard Subi, Mkurugenzi wa Kinga, aliyewataka wananchi kuvaa barakoa, kutumia vitakasa mikono na kunawa mikono kwa kutumia sabuni, ikiwa ni kanuni ya kinga, akidokeza kugundulika virusi vyake kutoka nchi jirani.

"Maambukizi yanaongezeka maradufu kuliko ilivyokuwa wimbi la pili," akafafanua.




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipozindua kampeni ya kitaifa kukabili maradhi ya UVIKO 19. **PICHA: MTANDAO.**

**HATUA KUBWA 2022**

Mnamo Machi mwaka, 2022 Rais Dk. Samia kwa mara nyingine akazungumzia hali ya maradhi Uviko 19, akisema serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, mashirika yasiyo ya kiserikali, taasisi za dini na wanataaluma wa afya, imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana na ugonjwa huo.

Hatua zake akazitaja zimezingatia mazingira na hali ya jamii, ikiwamo kuruhusu wananchi kuendelea kujitafutia kipato chao, yaani kutokuwapo vikwazo kama nchi nyinginezo.

Hiyo inatajwa hadi kufika Machi 2022, jumla ya watu 33,789 walishathibitika kuwa na maambukizi ya UVIKO - 19 na kati yao 803 walipoteza maisha nchini.

Hatua zilizochukuliliwa na serikali ni pamoja na kuwaondoa hofu wananchi mlipuko wa ugonjwa huu, kufunga shule, vyuo na taasisi za elimu ya juu.

Hiyo akaitaja inaendana na kutoa elimu kwa jamii namna ya kujikinga na kuhimiza jamii kusitisha mikusanyiko isiyokuwa ya lazima.

Vilevile akasema, kuimarishwa ukaguzi na uchunguzi wa afya kwa wasafiri katika viwanja vya ndege, bandarini na mipaka ya nchi kavu, kuzuia kuingizwa maambukizi mapya, huku kukiimarishwa mchango wa tiba asili.

Hayo yalikuwa yanafanyika katika Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii na Maabara katika Hospitali za Kanda za Bugando, Mbeya na Hospitali za Rufani za mikoa ya Dodoma, Arusha, Kigoma, na katika Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro.

Hiyo ikaendana na kusimikwa mitambo 15 ya hewa tiba ya Oksijeni katika hospitali mbalimbali nchini. Pia, serikali imeendelea kuikinga jamii kuwezesha upatikanaji wa chanjo.

Waziri akafafanua miaka mwili iliyopita; "Wananchi, narudia kusisitiza kuwa UVIKO-19 bado upo na hutokea kwa mtindo wa mawimbi yanayoambatana na mabadiliko mbalimbali. Kila mmoja wetu anao wajibu wa kushiriki katika mapambano dhidi ya ugonjwa huu.

"Nitumie fursa hii kuwashukuru sekta mbalimbali ndani ya serikali, wadau wa maendeleo, viongozi wa dini, viongozi wa kijamii na makundi mbalimbali ya kijamii kwa kutuunga mkono katika mapambano dhidi ya ugonjwa huu.

"Afya (Wizara) itaendelea kushirikiana na wote katika kuhakikisha tunaudhibiti ugonjwa huu. Hata hivyo, badala ya kupambana na ugonjwa huu peke yake, mwelekeo wetu sasa ni kuendelea

Inaendelea Uk. 12

AFYA

KUKITHIRI SHIDA AFYA AKILI...

# Bajeti tiba juu, Hospitali Mirembe yaboreshwa; kozi mpya zimeanza

**Na Yasmine Protace**

SHIDA ya afya ya akili ni ugonjwa unaotajwa kuenea kwa kasi kwa jamii, huku baadhi ya wanajamii hao hawana elimu inayohusu maradhi hayo.

Ni kawaida baadhi ya wanajamii wamekuwa wakihusishwa na matumizi ya dawa za kulevya zikiwamo bangi, hivyo wanaokumbwa wanachelewa kupata matibabu, sababu kuu ni wao kutojua sababu za ugonjwa huo na mawanda yake.

Hata hivyo, wataalamu wa afya ya akili wana ufafanuzi kwamba, ni ugonjwa unaoweza kumpata mtu yeyote, wakiwamo wasiotumia dawa za kulevya.

Shida ya afya ya akili zinatajwa inaweza kugundulika kwa mtu yeyote, hata wao bila ya kujijua kuwa anao.

Hapo inafafanuliwa kwamba, wapo wanaofika katika vituo vya afya wakiwa wanasumbuliwa na shida nyinginezo, lakini daktari anapompima vipimo mbalimbali, anagundua mgonjwa anakabiliwa na shida afya ya akili.

Inatajwa, wengi wanapogundulika na shida hiyo, ni wagumu kuamini kinachowasibu kiafya, wakidhani tatizo la afya ya akili ni kwa wanaotumia dawa za kulevya.

Hata katika mwonekano wao kimaumbile, huwa ni wa kawaida na watanashati, hata kuondoa imani kama wanasumbuliwa na shida ya afya ya akili.

Hilo linatoa mwelekeo kwa jamii kwamba, kunatakiwa kueleweka kwamba afya ya akili ni ugonjwa unaompata yoyote, sio lazima awe anatumia dawa za kulevya.

Hivi karibuni, serikali kupitia Wizara ya Afya imetenga kiasi cha mapato na matumizi katika bajeti ya mwaka 2024/25, kujenga chuo kikubwa na cha kisasa cha Afya - Mirembe cha uuguzi na ukunga.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anasema serikali hadi sasa imejitosheleza kwa vifaa vya kisasa na wataalamu katika eneo hilo la afya.

Waziri Ummy anasema hayo, alipofanya ziara katika Chuo cha Afya – Mirembe, kukagua hali ya chuo hicho na kuzungumza na wanafunzi chuoni hapo.

"Serikali imeona ipo haja ya kuongeza idadi ya wataalamu wa afya ya akili nchini Tanzania kwa kujenga hospitali kubwa na kuanzisha kozi ya mafunzo ya diploma ya juu ya uuguzi, ya utabibu wa afya ya akili.

Ni namna ya kuboresha upatikanaji wa wataalamu wa afya nchini, hata watakaosoma kozi hiyo kunufaika na mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Tanzania.

"Lengo letu ni kuhakikisha tunazalisha wataalamu wa afya ikiwamo wauguzi na wakunga wenye sifa, pamoja na ujuzi waliopikwa na wanaozingatia maadili ya kazi," anasema.

Anasema, lengo la serikali kupitia Wizara ya Afya ni kuanzisha diploma ya juu kwenye masuala ya saikolojia tiba, ili kusaidia watu wenye changamoto za afya ya akili, kutokana na ongezeko la idadi ya wenye changamoto hizo.

"Tunaona ongezeko la idadi ya watu wenye changamoto za afya ya akili, ambao takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), zinaonyesha kila watu nane mtu mmoja ana changamoto za afya ya akili," anasema.

Ufafanuzi wa WHO, ni kwamba afya ya akili mantiki yake ni dhana tofauti na 'uchizi', ikiangukia tafsiri pana katika changamoto hiyo.

Nchini Tanzania, takwimu za kiserikali zinarejea kuwapo wastani watu milioni 1.5 wanaousumbuliwa na afya ya akili, ikirejewa na shida ya maradhi sonona inayoongoza, ikifuatiwa na matumizi ya dawa za kulevya.

Aidha, Waziri Ummy anasema mwaka 2023 katika kukabili hali hiyo, Wizara ya Afya ilibuni mkondo wa masomo ya sayansi ya saikolojia tiba (Clinical Psychology).

"Nitumie fursa hii kuhimiza vijana kuomba kozi hii ambayo mwaka huu wa 2024/25 inaanza rasmi katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili (MUHAS) katika ngazi ya shahada (Degree)." anafafanua.

Anasema, dhamira ya serikali kupitia Wizara ya Afya, ni kuanzisha diploma ya juu, kwenye masuala ya saikolojia tiba katika Chuo cha Afya Mirembe, Dodoma, ili kuwasaidia wenye changamoto za afya ya akili, kutokana na ongezeko la wenye changamoto hizo.




Chuo cha Tiba Mirembe, Dodoma, kunakoanzishwa masomo tiba afya ya akili, kama ilivyo Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili (MUHAS), Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO.**

## Awamu ya Sita ilivyopokea 'hodi' UVIKO 19, hadi hatua ya 'baibai'

**INATOKA UK. 11**

kutoa huduma za kudhibiti Uviko -19 kupitia huduma nyingine jumuishi," anasema.

Hapo Waziri Ummy, anazifafanua kwa mifano ya tiba Kifua Kikuu, Huduma za Mama na Mtoto, huduma za VVU/UKIMWI, Malaria magonjwa yasiyoambukiza

Lakini hatua iliyofikiwa sasa ni kwamba, huduma hizo zinapatikana kila mahali, ikiwamo katika ngazi ya vituo vya afya takriban vyote, binafsi na vya serikali msingi wa hoja kama alivyotambulisha Rais Dk. Samia, ni ushiriki wa pamoja na uwezeshaji kufikisha huduma tajwa.

Hiyo katika sura ya pili inaundwa katika Sera ya Afya nchini, inayotokelezwa kwa karibu sana na Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), iliyobuniwa mwaka 2007 na kuanza kazi mwaka uliofuata.

**MPANGO& PESA UVIKO**

Kimsingi, dalili zake maradhi Uviko 19: -Homa kali; mgonjwa anajihisi kuchoka; anakohoa; anapata shida ya kupumua; vilevile kujihisi misuli imechoka.

Tanzania ilishawajibika na kunufaika na mradi wa miezi tisa, ilipotekeleza Mpango wa Serikali wa Kuinua Uchumi na Kukabiliana na Janga la Korona, uliopangiwa bajeti shilingi trilioni 3.62. Ulizinduliwa na Rais Dk. Samia, jijini Dodoma Oktoba, 2021.

Hapo Rais akaitaka Wizara ya Fedha na Mipango, pamoja na taasisi nyinginezo zitakazonufaika na fedha za mkopo wa shilingi trilioni 1.3 kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF), kuhakikisha zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Aidha, akaitaka sekta binafsi kutumia fursa hiyo, kwa kuzalisha bidhaa zitakazotumika katika utekelezaji wa miradi hiyo, mfano uzalishaji wa saruji, mabati na nondo, kusiwapo sababu ya kuchelewa kutumia fedha hizo.

Akaagiza miradi hiyo itekelezwe na makandarasi wazawa, ili fedha hizo ziendelee kubaki na kuzunguka katika uchumi wa nchi, huku akiwaelekeza makandarasi wazawa kuwajibika kwa tija.

Katika mpango huo, akataka kupunguzwa urasimu katika ununuzi wa vifaa vya miradi hiyo, agizo ilomfikia pia, Waziri wa Fedha na Mipango Dk. Mwigulu Nchemba kusimamia na kuondoa urasimu wa misamaha ya kodi katika vifaa na bidhaa zitakazotoka nje.

Vilevile, akamuagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) pamoja na Mkaguzi wa Hesabu za ndani, kufuatilia kwa karibu matumizi ya fedha hizo ili malengo na thamani halisi iweze kuonekana.

Pia, Dk. Samia akazitaka Kamati za Bunge, kuisimamia kikamilifu miradi hiyo wakati wa kuitembelea, agizo linalowashukia nao wakurugenzi wa halmashauri zote nchini, pamoja na timu zao za kazi, kuhakikisha wanasimamia vizuri fedha hizo zilete tija katika miradi hiyo.

Zao la yote hayo, ndio sasa linaibua ufafanuzi wa kuwapo matokeo na huduma zinazobeba jina 'Miradi ya fedha za korona.'

AFYA

BAADA YA NIPASHE KUANIKA...

# Zahanati iliyokwama miaka 14, hatimaye inajengwa kwa kasi

Na Marco Maduhu, SHINYANGA

Ni hadithi iliyochukua miaka 14 kusuasua ujenzi wa zahanati kijijini Mwamagunguli, Kata ya Kolandoto Manispaa ya Shinyanga, tangu mwaka 2010.

Baada ya Nipashe kuwasilisha mkasa wa kilio tajwa cha kukwama ujenzi miezi kadhaa kupita, ghafla hadithi imehamia kujengwa.

Ni simulizi inayoegemea Sera ya Afya ya Mwaka 1990, iliyorekebishwa mwaka 2007, ambao kisheria kukapitishwa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), ulioanza kutekelezwa mwaka 2008, ukihamasisha kushirikisha wananchi kuimarisha huduma za afya ngazi zote.

Sura iliyoko kimuundo, kila kijiji au mtaa nchini kinahitajika kuwa na zahanati na kituo cha afya kwa kila kata, huku wilaya ni hospitali.

Vivyo hivyo, mkoa na kanda kuwa na hospitali za rufani na kunakuwapo hospitali za kitaifa kama Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Taasisis ys Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI), Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete zote za Dar es Salaam, vilevile Benjamin Mkapa ya jijni Dodoma.

Sera MMAM inafafanua kwamba, wananchi washiriki kuanzisha ujenzi wa boma hadi hatua 'renta' za zahanati na kituo afya, serikali ikimalizia ujenzi.

Ndicho kilichojitokeza kijijini Mwamagunguli walijenga hadi 'renta' ya zahanati, lakini serikali imekwama ndani ya miaka 14 kukamilisha ujenzi kama wanavyoongozwa kisera.

**SERIKALI KIJIJINI**

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwamagunguli, Makoye Shindayi, anasema, sasa wamepokea shilingi milioni 50 kutoka Manispaa ya Shinyanga, Aprili mwaka huu, kumalizia ujenzi wa zahanati kijijini humo, kazi ya ujenzi ikiendelea sasa.

"Kwanza kabisa nakupongeza Mwandishi wa habari kwa kufika hapa kijijini mwezi wa tatu na kutuhoji juu ya boma hili la zahanati yetu kuchukua miaka 14 kushindwa kukamilika.

"Bila wewe kuirusha taarifa hii, huenda hata ujenzi usingeanza, lakini serikali imesikia kilio chetu kupitia wewe na ikatoa pesa (shilingi) milioni 50 na sasa kama unavyoona ujenzi unaendelea," anaeleza Mwenyekiti Shindayi.

Mkazi wao, Salome Ndaki, anasema kukamilika ujenzi wa zahanati hiyo na kuanza kutoa huduma, kutawasaidia kupata huduma umbali karibu, hasa kwa wajawazito wanaotaabika kutembea umbali mrefu kwenda kujifungua katika Hospitali ya Kanisa la AICT Kolandoto, akiamini sasa shida hiyo itaondokao.

Anatoa mfano, mjamzito anapopata uchungu usiku, inakuwa shida kumpeleka hadi Hospitali ya Kolandoto umbali mrefu, sasa anafaurahia mbadaa umepatikana.

"Tunaishukuru Serikali kwa kuanza kutukamilishia zahanati yetu hapa kijijini na itakuwa msaada mkubwa kwetu, hasa sisi wanawake ambao ndiyo huwa tunauhitaji mkubwa wa huduma za afya," anasema Salome.



Zahanati ya Mwamagunguli, Manispaa ya Shinyanga, ilivyokuwa awali. **PICHA ZOTE: MARCO MADUHU.**

Mwananchi, Hollo Jidula, anasema kukamilika zahanati hiyo inakuwa faraja kwao kiafya, ikiwamo kupata elimu ya afya ya uzazi Jirani na huduma ambazo hakuwazipata kirahisi, nje ya hospitali za kiserikali.

**WAHUDUMU AFYA**

Mhudumu wa Afya ngazi ya Jamii Kijijini humo. Ester Emmanuel, anasema kukamilika zahanati kunabaki kuwa mkombozi kwa wajawazito wakiondokana na adha ya kujifungua njiani na kuhatarisha maisha yao na mtoto.

Mganga Mkuu wa Manispaa ya Shinyanga Dk. Elisha Robert, anasema zahanati hiyo ya Mwamagunguli, itasaidia kuboresha upatikanaji huduma za afya kwa wananchi wa eneo hilo.

Anasema ujenzi wake uko katika hatua ya mwisho na tayari wameshapokea fedha za vifaa tiba kwa halmashauri, shilingi milioni 100, zikiwamo za zahanati Mwagala, inayoweza kufungfuliwa kati ya mwezi ujao na Agosti, kuanza matibabu.

"Tutakachokifanya ni kuhamisha watumishi wachache waende kwenye zahanati (Mwagala)," ili huduma zianze kutolewa,"anasema Dk.Elisha.

Diwani wa Kolandoto, Mussa Andrew, anaishukuru serikali kukamilisha kazo hiyo, akiamini ni msaada mkubwa kwa wananchi kijijini kupata huduma za matibabu karibu.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Alexius Kagunze, anasema kwa mwaka unaoisha 2023/2024, serikali kuu imeshatoa shilingi milioni 50 ili kukamilisha ujenzi wa Zahanati Mwamagunguli, fedha hizo zilishapelekwa sehemu husika kuendeleza ujenzi.



Zahanati ya Kijiji cha Mwamagunguli Manispaa ya Shinyanga, ujenzi unaendelea.

AFYA

## TAA KIJANI VITA UTAPIAMLO...

# Benki ya kuhifadhi mbegu za mboga miaka 100, ikinuwia aina 25,000

## •Pilipili nayo yavuma sokoni kivyake

**Na Mwandishi Wetu**

KUANZIA kauli ya Mkuu wa Taasisi ya Utafiti na Uendelezaji Mbegu za Mboga na Matunda Asili Bara la Afrika la World Veg, Dk. Gabriel Rugalema, anawahimiza wazalishaji mbegu za mboga na matunda kuzingatia ubora na matakwa ya soko, ili kuepuka hasara na wananchi kupata lishe bora na kutokomeza utapiamlo nchini unaosababishwa na lishe duni.

Dk. Rugalema ameyasema hayo, wakati akifungua mafunzo ya wazalishaji wa mbegu za pilipili na nyanya kutoka nchi za Afrika, katika makao makuu ya taasisi hiyo eneo la Tengeru wilayani Arumeru Mkoa wa Arusha.

Anasema mafunzo hayo kuhusu utafiti wa masoko ya mazao ya mboga na matunda akiwataka wazalishaji mbegu za mboga na matunda kuzalisha mbegu bora zinazoendana na mahitaji na matakwa ya soko, ili kuepuka hasara za masoko ya mazao yake.

"Soko ndio mfalme, mnapaswa kufahamu kuwa mahitaji ya wazalishaji wa mboga ndio msingi ili kuwawezesha kufikia malengo ya kibiashara na faida, mzingatie vigezo vya wateja wenu kama maumbo ya nyanya na pilipili wanayoyapenda ili kuwavutia walaji kukuza mnyororo wake wa thamani na kupata tija," anasema.

Kwa mujibu wa Dk. Rugalema, mbinu hizo ni muhimu kwa wazalishaji mbegu za nyanya na pilipili kuzifahamu, hasa Tanzania kutokana na soko lake kubadilika kwa kuwa inazalisha kwa ajili ya soko la ndani na nje.

Anasema utafiti ni kitu endelevu kibiashara na anatoa mfano katika miaka ya 1990, wao World Veg walizalisha mbegu bora za nyanya zilizovuma na kupendwa sehemu mbalimbali duniani.

Anazitaja baadhi ya nyanya hizo kuwa ni aina ya Tanya, Boko na Tengeru na kwa sasa zimepitwa na wakati, kutokana na walaji kutaka uzalishaji wa aina nyingine, ndipo wakazalisha Tengeru 97 hivi karibuni.

Anasema, taasisi yake inaendelea na utafiti wa ugonjwa wa mnyauko wa zao la nyanya, ili kuingiza mbegu mpya zitakazopambana na ugonjwa huo katika maeneo mengi ya Afrika.

Mkurugenzi huyo anasema takribani miaka mitatu, taasisi hiyo haijazalisha mbegu mpya ya nyanya na badala yake zilitumika mbegu mama kuzalisha aina nyingine ya kiungo hicho.

Anafafanua, mpango wa taasisi hiyo ni kutengeneza mbegu zinazomudu magonjwa, mabadiliko tabia nchi na changamoto za udongo.



Kilimo cha mboga mchicha kikiendelea shambani. **PICHA: MTANDAO.**

Mkurugenzi Msaidizi wa Mazao wa Wizara ya Kilimo, Beatrice Banzi, anasema World Veg ni mdau wao muhimu katika kuendeleza mazao ya bustani.

Beatrice, anasema mazao hayo yana umuhimu katika kuboresha programu za lishe nchini, kutokana na uhakika wa vitamini na madini baada ya kuzalishwa na kutunza kwa mbegu kwa ubora.

"Wenzetu hawa wanatushika mkono hapa nchini kwenye masuala ya utafiti na kuendeleza lishe bora," anaeleza, Mkurugenzi huyo, anayefafanua mafunzo hayo ni tunu ya taifa kutokana na kuhimiza wazalishaji wa mbegu wakifanya tafiti za masoko kutambua mahitaji ya wakati, kwa kiwango na penye mahiaji.

**WATAFITI MBOGA**

Mtafiti wa Pilipili Duniani, kutoka World Veg, Derek Barchenger, ana maelezo:

"Tunahakikisha pilipili tunazozalisha, zina uwezo wa kupambana na magonjwa lakini pia hazishambuliwi na wadudu."

Anasema, watumiaji pilipili wanapenda zenye ladha, harufu nzuri na muonekano wa kuvutia, hivyo anatoa jukumu la tafiti za kina kukidhi vigezo hivyo.

Bwanashamba Kiongozi wa asasi ya Kilele ya Sekta binafsi Tanzania, inayohusika na kuendeleza tasnia ya mboga na matunda, Gilian Daniel, anasema taasisi yake inatoa miongozo na mafunzo ya masoko na taarifa sahihi za kuwezesha kufahamu wakati wa kilimo ili kupata soko la uhakika.

Daniel anasema, taasisi ya Kilimo cha Mbogamboga na Matunda Nchini (TAHA) kwa kushirikiana na wadau wamelenga mafunzo hayo kuwa yatatosha kueneza taarifa kwa wakulima ili waondokane na kilimo cha mazoea.

"Wataalamu hawa zaidi ya 40 watakapotoka hapa, watafikisha taaluma hii kwa wakulima wengi zaidi na wao kujifunza namna nzuri ya kulima mazao kulingana na hali ya hewa na mahitaji mengine." anasema.

**BENKI YA MBEGU**

Nayo, Taasisi ya Utafiti wa vinasaba na Undelezaji Mbegu za Asili za mboga na matunda, imezindua benki maalumu ya kuhifadhi mbegu za mboga na matunda kwa miaka 100.

Ni benki inayotajwa kujengwa kwa gharama ya zaidi ya shilingi bilioni 1.2 ikifadhiliwa na China. pia Uholanzi, kijijini

Tengeru, wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha na itatumika kuhifadhi mbegu na kusambaza kwa wakulima na kampuni za mbegu barani Afrika.

Aina za mbegu za mboga na matunda zilizohifadhiwa na kuhifadhiwa ni mchicha lishe, bamia, ngongwe (nyanya chungu), mnafu, nyanya na vitunguu.

Akizindua benki hiyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Mweri ameonya isitumike kama makumbusho ya Taifa na kufungia mbegu na kutaka mbegu zilizotafitiwa na zenye ubora zisambazwe, ili kusaidia lishe bora kwa watu na tija kwa wakulima na maduka ya mbegu.

Mweri anasema, mbegu zinapotafitiwa na kuhifadhiwa vizuri, huvumilia ukame, kupambana na magonjwa na kupata mazao mengi.

Anasema moja ya changamoto ya dunia kwa sasa, ni kushindwa kuhifadhi mbegu zikiwa na ubora ule wa vitamini na madini, hivyo kusababisha utapiamlo kwa baadhi ya wananchi hususani watoto wadogo.

Mweri anasema benki hiyo imehifadhi aina 5,700 za mbegu na mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka huu itakuwa imehifadhi 11,000. Anasema lengo ni kuhifadhi aina 25,000 hadi kufikia mwaka 2025/26.

"Kuwapo Tanzania kwa benki hii bahati ya pekee kabisa, itasaidia vijana na wanawake kujiajiri kwenye mashamba ya bustani na hatimaye kujipatia vipato na kupunguza umaskini," anasema .

Mweri akaahidi kwamba, serikali itafanya tathmini ya kutoa eneo la ardhi ya kutosha wilayani Arumeru ilipo benki hiyo, ili kusaidia kupanua huduma zake kwa kitaifa na dunia.

"Nakubaliana na nyinyi, kituo hiki kinapanuka, shamba lililopo ekari 14 kwa ajili ya utafiti lilitolewa na serikali kwa World Veg miaka zaidi ya 31 iliyopita, halitoshi, tutatoa eneo kubwa litakalokidhi mahitaji lililopo karibu ili kupunguza gharama za kusafiri, "anasema.

Mkurugenzi Mkuu World Veg Afrika,Dk Rugalema, anasema kuzinduliwa benki hiyo kutapanua wigo wa uhamasishaji wanasayansi wa dunia, kutafiti zaidi na kupata ubora mkubwa zaidi na mbegu nyingine. Anasema, kituo hicho kimeipa heshima Tanzania kimataifa, kutokana na umuhimu wake kwa Afrika na Dunia.

Anasema mbegu zilizohifadhiwa, pia zinatumika kufundishia vikundi vya wanawake, vijana na wakulima katika mikoa mbalimbali nchini ili kuongeza fursa za ajira na kipato cha kaya.

Anataja aina ya nyanya inayofahamika kwa kina la Tengeru 97, iliyotafitiwa na kuhifadhiwa na World Veg. ambayo ndiyo inayotumika kwa mkoa wa Arusha na majirani kuwa inamudu kupambana na magonjwa, hali ya hewa na kuzaa mavuno mengi na bora.

"Tengeru 97 ni miongoni mwa mbegu zetu zinazotesa! Wakulima wengi na makampuni ya mbegu wanaitumia sana, sokoni inadumu muda mrefu bila kuharibika, ina ganda gumu na hayo ndio matokeo mazuri ya utafiti na utunzaji bora," anasema.





## NaCoNGO kupata viongozi wapya wiki ijayo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

BARAZA la Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), linatarajia kufanya uchaguzi mkuu Juni 25, mwaka huu, huku likiwataka wanachama kujitokeza kuchukua fomu na kurejesha kwa ajili ya kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Mwenyekiti wa kamati ya mpito ya kuratibu uchaguzi wa baraza hilo, Christina Ruhinda, alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa haabri kuhusu mchakato wa uchaguzi.

Ruhinda alisema kuwa katika mchakato huo tayari wajumbe 30 wa ngazi ya mkoa wamechaguliwa katika uchaguzi uliofanyika mwezi huu.

Alisema kati ya idadi hiyo wajumbe 26 ni washindi kutoka ngazi ya mkoa na wanne ni washindi kutoka makundi maalum ya wawakilishi wa mashirika yasiyo ya kiserikali ya watoto vijana na watu wenye ulemavu na kimataifa.

Alisema kuhusu uchaguzi wa ngazi ya taifa mwisho wa kuchukua fomu na kurudisha tayari umeanza na utafanyika kwa siku mbili na kamati itafanya kazi ya kuchambua fomu na kupitisha wagombea wasiozidi watatu katika kila nafasi.

Ruhinda alitaja nafasi ambazo zinawaniwa ni mwenyekiti, katibu mkuu, muweka hazina na wenyeviti wa kamati ndogo nne ambazo ni kamati za maadili, fedha na utawala maendeleo na uwezo na mawasiliano.

Nafasi zingine nne za uwakilishi wa baraza kwenye bodi ya uratibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali ambapo katibu mkuu wa baraza hilo anaingia kwa nafasi yake.

Alisema kwa wagombea wote wanaotaka kuomba nafasi hizo wanapaswa kujaza fomu na kuambatanisha nakala ya kiapo cha kiongozi katika ngazi ya mkoa na makundi maalumu na mashirika ya kitaifa.

# Wananchi London waomba kujengewa kituo cha afya

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

WANANCHI wa Kijiji cha London wilayani Manyoni mkoani Singida wameiomba serikali kuwajengea kituo cha afya kutokana na zahanati iliyopo kuzidiwa na idadi ya wagonjwa.

Walitoa ombi hilo juzi kwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake (UWT) mkoani Singida, Martha Kayaga wakati akiwa katika ziara ya kamati ya utekelezaji ya jumuiya hiyo mkoa ya kuimarisha na kuandikisha wanachama wapya.

Walisema kwa sasa zahanati ya London ina chumba kimoja tu ambacho kinatumika kwa wagongwa wote wanaofika hapo kupata matibabu.

Waliongeza kuwa wakati mwingine inawalazimu kufuta huduma za afya umbali mrefu hali inayosababisha madhara makubwa kwa kinamama na watoto ambapo wengine hupoteza maisha kabla hawajafika kwenye Kituo cha Afya Kata ya Makuru.

Mmoja wa wakazi wa Kijiji hicho, Asia Seif alikiri kujifungulia njiani na kupoteza maisha ya mtoto wake akiwa anaenda kituo cha afya ambacho kipo umbali wa zaidi ya kilomita 10 kutoka kijijini kwake.

Alisema iwapo serikali itajenga kituo cha afya katika kijiji hicho kutawaondolea adha wananchi ya kulazimika kutembea umbali mrefu kufuata huduma katika Kituo cha Afya Makuru.

Wananchi hao pia waliiomba serikali kuongeza idadi ya watumishi kwani waliopo ni wachache na wakati mwingine wagonjwa wakiwa wengi inalazimu mgonjwa mwingine asubiri mpaka amalize, hali ambayo ni hatari endapo kuna mgonjwa anatakiwa kupata huduma kwa haraka.

Diwani wa Viti Maalum kutoka Kata ya Kilimatinde, wilayani Manyoni, Magreth Richard alikiri kuwepo kwa changamoto hiyo katika kijiji hicho kuhudumia vijiji vinne na hivyo kuzidiwa idadi ya wagonjwa.

Alisema kuna wakati chumba hicho kimoja kilichopo kinawalaza kinamama na kinababa kwa wakati mmoja, huku wengine wakiwa wamelala chini, jambo ambalo sio zuri la kuwalaza watu wa jinsia mbili tofauti katika chumba kimoja.

Akijibu maombi hayo, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake UWT Mkoa wa Singida, Kayaga aliwataka wananchi hao kuwa wavumilivu kwamba serikali inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo kujenga vituo vya afya ili kuondoa changamoto zinazowakabili wananchi.

Alisema changamoto hiyo anazichukua na kuzifikisha mahala husika ili waje kuona namna ya kujenga kituo hicho cha afya.

Aidha, aliwataka wananchi hao kutenga eneo mapema ili serikali itakapoamua kujenga kituo hicho cha afya kusiwe na kisingizio na liwe na hati miliki ili kuondoa migogoro wakati wa ujenzi.



Naibu Waziri Katiba na Sheria, Jumanne Sagini (kulia), akijadiliana jambo na Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Stanslaus Nyongo (kushoto) na Mbunge wa Jimbo la Mbagala, Abdallah Chaurembo, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wamiliki vituo vya afya watakiwa kuzingatia kanuni

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imewataka wamiliki wa taasisi na maeneo ya kutolea huduma za afya kuzingatia kanuni za vibali vyao, ikiwa ni pamoja na kutumia wataalamu wenye sifa na waliosajiliwa ili kulinda afya ya wananchi.

Pia, imewataka wamiliki wa maduka ya dawa nchini kufuata masharti ya leseni zao za kufanya biashara ili wasihatarishe afya za wananchi.

Rai hiyo ilitolewa na Meneja wa TMDA Kanda ya Kati, Sonia Mkumbwa wakati akitoa msaada wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi vyenye thamani ya Sh. milioni 24 kwa Gereza Kuu la Isanga mkoani hapa.

Mkumbwa alisema kuwa dawa hizo zimepatikana kwenye msako unaofanywa na mamlaka hiyo kwenye maduka ya dawa na vitendanishi, ambavyo vimekuwa vikihifadhiwa maeneo ambayo siyo sahihi.

Alisema zipo taratibu na masharti ya kuhifadhi dawa hizo, hivyo ni lazima wanaotoa huduma za dawa za binadamu kuzifuata ili ziendelee kuwa katika hali nzuri bila kuleta madhara kwa binadamu.

"Kawaida kila dawa ina mazingira yake ya kuhifadhiwa na dawa nyingi zinatakiwa kuhifadhiwa kwenye joto lisilozidi nyuzi 30 na nyingine zinatakiwa kuhifadhiwa kwenye majokofu, lakini dawa hizo zilikutwa zimehifadhiwa kwenye mazingira ambayo siyo salama na kama zingeachwa zingeleta madhara kwa mtumiaji," alisema.

Alitaja dawa ambazo zimepelekwa kwenye gereza hilo kuwa ni za kupunguza maumivu, antibiotiki, shinikizo la damu na zingine za vidonda.

Alisema dawa hizo bado zipo kwenye hali nzuri kwa ajili ya matumizi ya binadamu na hivyo zinaweza kutumika bila shida yoyote.

Mkuu wa Gereza hilo, Zefania Neligwa, alisema msaada huo wa dawa umekuja kwa wakati kutokana na kupokea watu wenye matatizo mbalimbali ya kiafya, huku wengine wakija na majeraha makubwa yanayohitaji matibabu.

Neligwa alisema kuwa gereza hilo lina wafungwa 1,147 na askari magereza 343 ambao wote wanategemea huduma za matibabu kutoka kwenye zahanati iliyopo kwenye gereza hilo, hivyo msaada huo umekuja kwa wakati.

Daktari wa zahanati iliyopo kwenye gereza hilo, Pantaleo Maumba alisema dawa hizo ni msaada mkubwa kwani wanahudumia idadi kubwa ya mahabusu na wafungwa.

Alisema msaada huo utatumika kama ulivyokusudiwa na kuiomba TMDA kuendelea kutoa msaada wa vifaa tiba na dawa kwani mahitaji bado ni makubwa.





# Watishia kushiriki uchaguzi kisa ukosefu wa umeme

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

WANANCHI zaidi ya 1,300 kutoka vitongoji vya Nyamagana na Itulahumba wilayani Wanging'ombe mkoani Njombe wamesema hawaoni sababu ya kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu, kutokana na vitongoji vyao kutokuwa na umeme.

Wakizungumza na Nipashe wananchi hao walisema licha ya uwepo wa mpango wa usambazaji wa umeme vijijini lakini katika kata yao bado vitongoji vyao havijafikiwa na umeme, licha ya vitongoji vya vijiji vingine jirani kufikiwa na huduma hiyo.

Walisema hawaoni umuhimu wa kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu kwa sababu viongozi hawawapi ushirikiano.

Wananchi hao akiwemo, Alex Mhagama alisema hivi sasa watoto wao wanakosa masomo ya jioni kutokana na kukosekana kwa umeme.

"Kizazi cha sasa kinategemea sana elimu, kwa hiyo kama kiongozi anahitaji kuchaguliwa basi asimame na sisi kwa sababu tunahitaji umeme," alisema Mhagama.

Wema Mfilinge alisema kukosekana kwa umeme katika maeneo yao kunasababisha wakose huduma za msingi ikiwemo viwanda na kusababisha kutokukuwa kwa uchumi wao.

"Hata kwenye kusaga unga tunakwenda mashine za mbali sana. Wengine wana cherehani zinatumia umeme lakini wanashindwa kuzitumia kwa sababu hakuna umeme," alisema Mfilinge.

Diwani wa Kata ya Itulahumba, Thobias Mkane alisema ni kweli vitongoji hivyo havijafikiwa na mpango huo na kueleza kuwa jitihada zinaendelea ili kuhakikisha vinafikiwa na umeme.

"Mpaka sasa hivi kuna vitongoji havijafikiwa na umeme kabisa ni vitano lakini vingine vimefikiwa katika kata yangu, nina vitongoji 15, mpaka sasa hivi tumeshapeleka umeme kwenye vitongoji 11 kwa hiyo tumebakiza vitongoji hivi vinne ama vitano kwa ajili ya kuhakikisha tunamaliza," alisema Mkane.

Naye Mratibu wa Miradi ya Usambazaji wa Umeme Vijijini (REA) Wilaya ya Wanging'ombe, Justine Dickson alisema kwa awamu ya pili B vitongoji 75 ambavyo vimepitiwa na laini kubwa ya umeme vitafikiwa na huduma ya umeme jazilizi na kueleza kuwa mpango wa serikali ni kuhakikisha wananchi wote wanafikiwa na umeme katika awamu ya pili C.





Mkurugenzi wa Jukwaa la Wapigapicha za Mnato na Video Tanzania, Rajab Mchatta akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu kongamano la mwaka la jukwaa hilo, linalotarajiwa kufanyika Juni 25 mwaka huu Mbezi Garden. Kulia ni mmoja wa wadhamini wa kongamano hilo, Msimamizi wa Masoko wa Chenga ED, Tumaini Kaberege. **PICHA: JOHN BADI**

# Mbaroni tuhuma mauaji mama mzazi, dada

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe linamshikilia, Simon Mtitu (29) mkazi wa Lugarawa wilayani Ludewa kwa tuhuma za mauaji ya mama yake mzazi pamoja na dada yake.

Hayo yalisemwa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Mahamoud Banga wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani hapa.

Alisema mtuhumiwa huyo alifanya mauaji hayo kwa kumpiga mama yake na dada yake kwa vitu vizito kichwani likiwemo jembe alilokutwa nalo siku ya mazishi.

Kamanda Banga alisema chanzo cha mauaji hayo ni kuwa mtuhumiwa huyo ana matatizo ya afya ya akili ambapo siku za nyuma aliwahi pia kushtakiwa kwa kosa la ubakaji lakini hakupatikana na hatia.

Alisema mtuhumiwa huyo baada ya kurejea nyumbani alihamishia matukio hayo ya ubakaji kwa dada yake kwa kumuingilia pale anapokuwa na matamanio ya haja zake za kimwili.

Alibainisha kwamba kitendo hicho kilimlazimu mama yake mzazi kumzuia ndipo mtuhumiwa huyo akatekeleza mauaji hayo.

"Kwahiyo mtuhumiwa tumekamilisha upelelezi wake na atafikishwa mahakamani muda wowote kuanzia sasa," alisema Banga.

Wakati huo huo, Kamanda Banga alisema Jeshi la Polisi linamshikilia Albert Mtewele (58) mkazi wa Kijiji cha Mlevela wilayani Wanging'ombe kwa kukutwa na pikipiki nne za wizi.

Alisema kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo ni baada ya kufanyika kwa operesheni iliyofanikisha kukamatwa kwa pikipiki zingine mbili mkoani Morogoro ambazo zilihusika katika mauaji ya madereva bodaboda wawili huko Makambako mkoani Njombe.

Alisema watuhumiwa wawili wamekiri kutenda makosa hayo likiwemo tukio la kuuawa kwa mlinzi kwenye minara ya kampuni za simu eneo la Makambako.

Alisema katika tukio lingine, Jeshi la Polisi linamshikilia Jimson Godfrey (32) kwa tuhuma za kuunganisha nyaya za umeme wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) bila ya kufuata utaratibu.

"Huyu mtu ni kishoka anatafuta wateja na akipata anaenda kuwaunganishia umeme na anamuwekea mita ya luku ya zamani ambayo mwisho wa siku umeme unapita moja kwa moja," alisema

Kadhalika, alitoa wito kwa wananchi mkoani Njombe kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi na elimu hiyo itaendelea kutolewa kupitia vikao vya polisi jamii.

Baadhi ya wakazi Njombe wakitoa maoni yao akiwemo Godfrey Msigwa alisema changamoto kubwa ya kukikithiri kwa mauaji mkoani Njombe kunasababishwa na uwepo wa imani za kishirikina na kukosekana kwa elimu miongoni mwa wanajamii.

Alisema: "Sababu kubwa ni imani za kishirikina ambayo inatokana na watu kukosa elimu ambapo watu wanakwenda kwa waganga kwa kuaminishwa ukiua unapata utajiri jambo ambalo siyo kweli".

## Wapendekeza wanaochoma misitu wapewe adhabu kali

**Na Elizabeth John,** MAKETE

WANANCHI wilayani Makete mkoani Njombe, wameomba serikali kuchukua hatua kali kwa watu wanaochoma moto misitu na kusababisha uharibifu wa mazingira.

Walitoa ombi hilo kwa kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa, Godfrey Mnzava.

Walisema athari za moto kichaa ni kubwa kwa sababu zinadhoofisha uchumi wa mwananchi mmoja mmoja kutokana kuunguza sehemu kubwa ya ardhi.

Getord Msigwa mkazi wa Kijiji cha Ndulamo alisema wanaiomba serikali kuwasaidia kudhibiti tatizo la uchomaji moto misitu kiholela kwa sababu linawapa hasara.

Yohana Chengula mkazi wa Kijiji cha Mang'oto alisema wanaharibu mazingira kupitia kuchoma moto ovyo katika misitu yao.

Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa, Godfrey Mnzava aliwaagiza wataalam wa idara ya maliasili na mazingira wilayani Makete kuwasilisha taarifa juu ya hatua walizochukua dhidi ya matukio ya uchomaji moto kiholela.

"Kwanini wanaendelea kuchoma moto miti, kwanini wanaendelea kuchoma misitu? naomba taarifa ya kuona kwamba mnapambanaje. Pia naomba taarifa ya watu waliokamatwa kwa kuhusika kuchoma moto na hatua zilizochukuliwa wanapoharibu mazingira," alihoji Mnzava.

Ofisa Maliasili na Mazingira Halmashauri ya Wilaya ya Makete, Upendo Mgaya alisema wilaya hiyo wanakabiliwa na tatizo la uchomaji moto misitu.

Alisema: "Ili kukabiliana na tatizo la uchomaji moto tumekuwa tukitoa elimu kupitia mikutano ya hadhara, hivyo tunaendelea kutoa elimu ya uchomaji moto katika makundi mbalimbali"

Mkuu wa Wilaya ya Makete, Juma Sweda akipokea Mwenge wa Uhuru wilayani hapa alisema Mwenge huo utakimbizwa kwenye miradi nane yenye thamani ya Sh. bilioni 1.4.



# Matukio ajali barabarani yashika kasi Zanzibar

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

MATUKIO ya ajali za barabarani Zanzibar yameongezeka kwa asilimia 11.1 katika kipindi cha Mei mwaka huu na kufikia 20, kulinganisha na ajali 18 kwa kipindi cha Aprili mwaka huu.

Mtakwimu kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Ahmada Suleiman aliyesema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari na kueleza kuwa Wilaya ya Kaskazini A imeripotiwa kuwa na ajali nyingi zaidi.

Alisema kuwa ukilinganisha na ajali za barabarani kwa mwaka 2023 na Mei mwaka huu, idadi hiyo imeongezeka kwa asilimia 66.7 na kufikia ajali 20 kwa Mei mwaka 2024 kutoka ajali 12 kwa kipindi cha Aprili 2023 mwaka jana.

Alisema kuwa jumla ya waathirika 25 waliripotiwa kwa kipindi cha Mei mwaka huu ambapo waathirika 20 ni wanaume na waathirika watano ni wanawake.

Alisema kuwa katika ajali hizo waliofariki kwa kipindi cha Mei mwaka huu waliongezeka kwa asilimia 7.7 kufikia 14 kwa mwezi huo kutoka waathirika 13 waliofariki katika kipindi cha Aprili 2024.

Alisema kuwa waliojeruhiwa katika ajali hizo kwa mwezi uliopita walipungua kwa asilimia 56.0 na kufikia waathirika 11, waliojeruhiwa kwa Mei 2024 kutoka waathirika 25 kwa kipindi cha Aprili 2024.

Alieleza kuwa waathirika waliofariki kwa Mei 2024 wameongezeka hadi kufikia 14 kwa kipindi cha Mei 2024 kutoka waathirika sita kwa kipindi cha Aprili 2024 mwaka huu.

Alisema kuwa waliojeruhiwa kwa kipindi cha Mei mwaka huu wamepungua kwa asilimia 50.0 na kufikia waathirika 22 waliojeruhiwa kipindi cha Mei mwaka jana.

Alisema chanzo cha ajali hizo ni mwendo kasi wa madereva pamoja na uzembe, makosa 3,464 yameripotiwa kwa kipindi cha Mei mwaka huu, kwamba makosa 3,453 yaliripotiwa kwa wanaume na makosa 11 kwa wanawake.

Sajenti Ali Abdallah kutoka makao makuu ya Jeshi la Polisi Zanzibar alisema bado kuna changamoto kubwa kwa wananchi kutofahamu sheria za usalama barabarani hasa waenda kwa miguu.

Alisema lazima jamii ikubali kutoa mchango hasa wazazi kutowanunulia watoto wao vyombo vya moto wakati hawana leseni.

# Viongozi wa mabunge duniani kukutana Z'bar

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

VIONGOZI wa Kamati wa Umoja wa Mabunge Duniani wamekutana visiwani Zanzibar kujadili mambo mbalimbali ambayo yanahitaji kufanyiwa maamuzi.

Akizungumza na waandishi wa habari eneo la Kizimkazi visiwani Zanzibar kabla ya kuanza kwa vikao vyao, Rais wa Umoja wa Mabunge Dunia (IPU), Dk. Tulia Ackson alisema viongozi lazima wakutane kabla ya kuanza kwa mkutano wa IPU ambao unatarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu jijini Geniva.

Alisema mambo watakayojadili ni maandalizi ya mkutano huo pamoja na masuala yanayopaswa kufanyiwa maamuzi ikiwemo taratibu mbalimbali ambazo zinahitaji kurekebishwa ndani ya bunge hilo hususani masuala yanayosumbua Afrika.

Alisema moja ya mambo yanayosumbua kwa Afrika ni kutojadiliwa kwa hoja zao kutokana na kukosa nguvu ya kura, hivyo kikao hicho kitajadili suala hilo ili maamuzi yachukuliwe na kufanyiwa mabadiliko.

"Mkutano wa Umoja wa Mabunge Duniani huwa unawakutanisha wabunge zaidi ya 2000 kwa wakati mmoja. Hivyo tunapokuwa na kundi kubwa la namna hiyo wakati mwingine watumishi wa Bunge huwa wanapata changamoto ya kijinsia kutoka kwa wabunge au wakati mwingine wabunge kwa wabunge hupata athari" alisema Dk. Tulia.

Aidha, alisema viongozi wameona suala hilo ni jambo mojawapo la kutilia mkazo ili kutoogopa kuhudhuria mkutano kwa sababu ya usumbufu wa kijinsia.

Dk. Tulia alisema pia watajadili mkutano mkubwa wa maspika wa dunia nzima wa mabunge wa umoja duniani ambao hufanyika mara moja kwa muda wa miaka mitano, hivyo aliwataka Watanzania kuendelea kutoa maoni mambo gani wangependa maspika wa dunia nzima kuyajadili.

Alisema mojawapo ya msuala ya kujadili ni hoja ya umasikini ambapo nchi zingine zinaendelea vizuri lakini nyingine zipo kwenye wimbi la umasikini na mojawapo ya visababishi ni vita vinavyoendelea.

"Wote tunafahamu kuwa baraza letu linachangamoto ya vita katika nchi mbalimbali ikiwemo DRC, Sudan, nchi za Afrika Magharibi na mambo kama hayo tungependa kujadiliwa na maspika wa mabunge ya dunia nzima"alisema.

Dk. Tulia alisema kwa sasa nchi 180 zipo katika IPU na sasa wanahitaji nchi za Umoja wa Mataifa (UN) nazo kuingia katika umoja wa mabunge duniani, hivyo kupitia kikao hicho watapata fursa ya kujadili nchi zingine kuwa nazo kwenye umoja huo.

Alisema zipo baadhi ya nchi zinashindwa kulipa kiingilio cha Umoja wa Madola Duniani, hivyo watajadili namna bora ya kushirikiana nao ili kutowaacha nyuma kwa sababu kila nchi ina bunge na wanatamani kushiriki kwenye umoja huo.




Mwakilishi wa Jimbo la Mtambwe, Dk. Mohammed Ali Suleiman, akichangia mada katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Zaidi ya watu 35 waugua ugonjwa wa ngozi

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema inatambua uwepo wa ugonjwa wa maradhi ya ngozi visiwani hapa, kwamba mpaka sasa kuna wagonjwa 35 wanaougua, kati ya hao 12 wapo Unguja na 23 Pemba ambao wanaendelea na matibabu.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Afya, Hassan Khamis Hafidh katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa Mtambwe, Dk. Mohammed Ali Suleiman.

Mwakilishi huyo alitaka kujua, Je? Serikali inatambua uwepo wa ugonjwa huo, na takwimu zipo vipi kuhusu wagonjwa wa ugonjwa huu hadi sasa.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema ugojwa huo ni wa kurithi na husababishwa na shida inayotokana na vinasaba ambapo ngozi ya mgonjwa hushindwa kurekebisha athari zitokanazo na jua.

Alisema ugonjwa huo huleta athari katika ngozi yake na kuwa na mabaka na hata kupelekea saratani ya ngozi wakiwa na umri mdogo.

Alisema serikali inaendelea kuwahudumia watoto hao kupitia wataalamu wa magonjwa ya ngozi na kuhakikisha familia zinapatiwa elimu juu ya maradhi hayo, vifaa tiba kama dawa za mionzi ya jua na kupunguza saratani.

Vile vile, alisema changamoto kubwa wanayopata watoto hao ni uangalizi maalumu kutoka kwa wataalamu wa ngozi mara kwa mara, hata hivyo serikali imejipanga kuwatumia madaktari bingwa wa ngozi ili waweze kuwafanyia uchunguzi watoto hao mara kwa mara.

"Mheshimiwa Spika, serikali imejipanga kushirikiana na wataalamu wa ngozi kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja na KCMC ya Moshi kufanya kambi za maradhi ya ngozi kwa watoto hawa kila baada miezi mitatu ili kuwapunguzia gharama za usafiri na shida zitokanazo na maradhi hayo" alisema.

Katika hatua nyingine akijibu swali la mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Ameir Abdallah aliyetaka kujua tathmini ikoje juu ya ongezeko la tatizo la saratani ya shingo ya kizazi, Naibu Waziri huyo alisema tathmini inaonyesha kuwa tatizo la saratani ya shingo ya kizazi linaongezeka visiwani Zanzibar.

Alisema kinamama 69 wamegundulika kuwa na saratani ya shingo ya kizazi mwaka 2022/2023 na kufikia kinamama 105 wenye tatizo hilo mwaka 2023/2024.

Alisema mwanamme ndiye msafirishaji mkubwa wa kimelea cha saratani ya shingo ya kizazi kutokana na kuwa na tabia ya kuwa na wenza wengi anaofanya nao mapenzi, hivyo ni rahisi kuchukua kimelea hicho kwa mtu mmoja na kupeleka kwa mwengine.

HABARI KIMATAIFA

# Ramaphosa aapishwa kwa muhula wa pili

**PRETORIA,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, ameapishwa mjini Pretoria kuhudumu katika wadhifa huo kwa muhula wa pili.

Hatua inayokuja baada ya Chama chake cha African National Congress (ANC), kuafikiana na vyama vya upinzani kuunda serikali.

Hafla hiyo imeongozwa na Jaji Mkuu kwenye taifa hilo, Raymond Zondo, maofisa wengine wa serikali pamoja na viongozi wa kidini na kitamaduni pia wamehudhuria kuapishwa kwa Ramaphosa.

Ramaphosa, aliingia madarakani kwa mara ya kwanza mwaka wa 2018 baada ya mtangulizi wake Jacob Zuma, kulazimika kusitisha muhula wake kutokana na tuhuma za ufisadi.

Alichaguliwa tena kuongoza Afrika Kusini kwa muhula wa miaka mitano mwaka wa 2019.

Nchini Afrika Kusini, wapigakura wanawachagua wabunge ambao baadaye hupiga kura kumchagua rais.

Kwa mara ya kwanza tangu kuanza kwa demokrasia nchini Afrika Kusini mwaka wa 1994, Chama cha ANC kilipoteza wingi wake katika bunge la kitaifa.

Wabunge wiki iliyopita walipiga kura kumchagua tena kiongozi huyo mwenye umri wa miaka 71 baada ya uchaguzi wa Mei 29, mwaka huu, kukosa kutoa mshindi wa moja kwa moja.

Viongozi mbalimbali kutoka mataifa ya Afrika akiwamo Rais wa Nigeria, Bola Ahmed Tinubu, Joao Lourenco wa Angola, Denis Sassou Nguesso kutoka Congo Brazzaville na mfalme wa Eswatini Mswati III na Waziri Mkuu wa zamani wa Kenya Raila Odinga, wamehudhuria hafla hiyo.

Hii imekuwa mara ya tatu kwa Ramaphosa kuapishwa.

Wabunge walimchagua tena kusalia kama rais wiki iliyopita kufuatia makubaliano ya kuunda serikali ya mseto kati ya ANC, mpinzani wake wa muda mrefu wa Democratic Alliance (DA) na vyama vingine.

Sherehe hizo, katika siku ambayo ofisi ya rais inasema ni siku ya kawaida ya kazi, itajumuisha maonyesho ya muziki na kisanii, salamu ya bunduki 21, ndege za kijeshi na maandamano yaliyopita na vikosi vya ulinzi vya nchi hiyo.

Chama cha uMkhonto weSizwe (MK), kilichoundwa miezi sita iliyopita na Rais wa zamani Jacob Zuma, kimesema maofisa wake hawatashiriki katika hafla ya kifahari.

Chama hicho, ambacho kilipata asilimia 15 ya kura na kupata viti 58 vya ubunge, pia kilisusia kikao cha kwanza cha bunge Ijumaa iliyopita.

Ramaphosa amesalia na kiti cha urais ingawa ANC ilipoteza asilimia 17 ya kura na viti 70 bungeni.

ANC ilipata asilimia 40 ya kura, huku DA ikishika nafasi ya pili kwa kupata asilimia 22.

Muungano huo ni kuelekea kwenye kituo cha kisiasa, kwa sababu vyama vya mrengo wa kushoto vya ANC na vyama vilivyojitenga na wafuasi wengi vilikataa mwaliko wa kujiunga na serikali ya umoja wa kitaifa.

Ramaphosa anatarajiwa kuteua baraza la mawaziri punde tu baada ya kuapishwa, ambalo litajumuisha washirika wake wapya wa muungano - DA na vyama vingine vitatu vidogo.

Kwa pamoja, muungano huo unachukua asilimia 68 ya viti bungeni.

Rais pia anatarajiwa kutangaza ajenda ya kuokoa uchumi unaodorora.

*RFI*



Rais Cyril Ramaphosa (kulia), akiapa kushika wadhifa huo kwa muhula wa pili, akiongozwa na Jaji Mkuu Raymond Zondo, mjini Pretoria, nchini Afrika Kusini jana. **PICHA: SABC**

## Watu 200 wakamatwa kupinga ongezeko la kodi

**NAIROBI,** KENYA

ZAIDI ya waandamanaji 200 wamekamatwa katika mji mkuu wa Kenya, Nairobi, katika maandamano yanayoendelea ya kupinga mapendekezo ya kuongeza kodi.

Muswada wa sheria ya fedha unatarajiwa kuwasilishwa bungeni.

Mashirika ya kiraia yalisema maandamano hayo na mpango wa waandamanaji kukaa nje ya majengo ya bunge, utaendelea licha ya kukamatwa kwa waandamanaji 210.

Kamanda wa Polisi wa Nairobi, Adamson Bungei, alisema hakuna kundi lolote lililopewa kibali cha kufanya maandamano katika mji mkuu huo.

Wakenya wamehakikishiwa haki ya kuandamana kwa amani katika katiba.

Bungei alisema waandaaji wa maandamano wanatakiwa kuwaarifu polisi mapema, kitu ambacho hawakufanya.

Polisi walitumia mabomu ya kutoa machozi kuwasambaza mamia ya waandamanaji siku ya Jumanne, Juni 18, mwaka huu, hali iliyowalazimisha wafanyabiashara kufunga biashara zao kwa muda kwa kuhofia mali zao kuporwa.

Baadhi ya mapendekezo ya kuongeza ushuru katika muswada huo, yalitupiliwa mbali siku ya Jumanne, baada ya wabunge wa chama tawala kufanya mkutano na Rais William Ruto.

*BBC*

**Bungei alisema waandaaji wa maandamano wanatakiwa kuwaarifu polisi mapema, kitu ambacho hawakufanya.**

# Kim Jong Un: Uhusiano wetu umefika viwango vya juu

**PYONGYANG,** KOREA KASKAZINI

RAIS wa Korea Kaskazini, Kim Jong Un, amesema uhusiano kati ya nchi yake na Russia, umefika viwango vya juu na kwamba nchi yake inalenga kuuimarisha zaidi.

Matamshi ya Rais Kim Jong, yamekuja wakati huu mwenzake Vladimir Putin, amezuru nchini Korea Kaskazini.

Rais Putin yupo nchini Korea Kaskazini, kuimarisha ushirikiano kati ya mataifa hayo mawili yenye silaha za nyuklia, ziara inayokuja wakati huu Moscow ikiendelea kuivamia Ukraine.

Uhusiano wa Moscow na Pyongyang, umezua wasiwasi kutoka kwa mataifa ya Magharibi ambayo yanaamini kwamba, Russia imekuwa ikitumia silaha kutoka Korea Kaskazini kutekeleza mashambulio nchini Ukraine.

Chini ya utawala wake, ukuaji wa kiuchumi umeendelea kudorora, huku kukiwa na kukatwa kwa umeme, kuongezeka kwa uhalifu na ukosefu wa ajira.

Rais Putin amekaribishwa rasmi nchini Korea Kaskazini baada ya kuwasili Pyongyang usiku wa manane.

Alilakiwa katika uwanja wa ndege na kiongozi huyo.

Vyombo vya habari nchini humo, vinaripoti kuwa viongozi hao wawili walijadili namna ya kuimarisha mahusiano na kile wanachokitaja kubadilishana mawazo. Hii ni ziara ya kwanza ya Rais wa Urusi nchini Korea Kaskazini kwa kipindi cha miaka 25.

Russia, inapokea silaha nzito ikiwamo makombora ya masafa marefu kutoka kwa Korea Kaskazini, nayo ikiipa chakula, nishati, teknolojia miongoni mwa vingine.

Kulingana na utabiri wa hali ya hewa wa BBC kutakuwa na jua huko Pyongyang katika saa zijazo kwa hivyo hakuna uwezekano wa mvua kunyesha - hali nzuri kwa mapokezi ya serikali.

Hayo yatafuatiwa na mazungumzo ya kidiplomasia, pamoja na kutembelea kanisa la Orthodox miongoni mwa mambo mengine.

Pia inatarajiwa kuwa wawili hao watatia saini makubaliano mbalimbali, kuanzia uchumi hadi usalama.

*BBC*

# Singida yageukia madeni ili kusajili

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Singida Fountain Gate, imekiri kuwa inadaiwa kama ilivyoeleza taarifa ya Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), iliyotoka jana, ikaahidi kulipa madeni yote ndani ya wakati ili ipate ruhusa ya kusajili.

Rais wa klabu hiyo, Japhet Makau, amesema hayo siku moja tu baada ya TFF kutoa taarifa ya kuzizuia klabu tano ikiwamo timu yake kusajili mpaka itakapowalipa wachezaji wanaozidai.

"Ni kweli tunajua tuna madeni hayo na tunatakiwa kuyalipa, tatizo lilianzia msimu uliopita, tulikuwa na wachezaji wengi na tulikuwa na matatizo katika kuwalipa, tukaanza kufanya mabadiliko ya kuwapunguza, lengo lilikuwa ni hilo kupunguza matumizi makubwa na kukabiliana na hayo madeni, kwa hiyo tunayatambua na tumetengeneza mikakati ya kuyamaliza kwa muda mfupi ili tuweze kusajili wachezaji wapya," alisema.

Alisema kwa sasa wanaendelea kuingia mikataba na wachezaji wapya mbalimbali ambao wataitumikia timu kwa msimu ujao, lakini haiwezi kuwaingiza kwenye mfumo hadi hapo itakapomaliza kuwalipa wachezaji wanaodai.

**"Hivi sasa tumeshaanza kuingia mikataba na baadhi ya wachezaji, lakini suala la kuingiza kwenye mfumo litakuja muda si mrefu kwa sababu kwa sasa hatuwezi, wametuzuia, ila tuna miezi miwili mbele, kila kitu kitakaa sawa na kwa hili ilitokea msimu uliopita, tumejifunza, nadhani baada ya hapa hakutatokea tena jambo hilo," aliahidi.**

Taarifa iliyotolewa juzi na (TFF), ilieleza shirikisho hilo pamoja na Shirikisho la Kimataifa la Mpira wa Miguu (FIFA), limezizuia timu tano kusajili, hivyo haziwezi kuingiza mchezaji yeyote kwenye mfumo wa usajili wa kimataifa.

Klabu hizo ni Yanga, Singida Fountain Gate, Tabora United, Biashara United na FGA Talents.

"Klabu ambayo itawalipa wahusika, itaondolewa mara moja adhabu ya kufungiwa kusajili," ilieleza sehemu ya taarifa hiyo.

Katika taarifa yake hiyo, TFF ilisema mpaka juzi asubuhi, hakuna klabu yoyote kati ya hizo iliyowalipa wahusika, ikiwakumbusha kufanya hivyo, vinginevyo hawatoweza kufanya usajili.

# MEXIME APEWA MIKOBA YA BARAZA DODOMA JIJI FC

Na Shufaa Lyimo

UONGOZI wa Klabu ya Dodoma Jiji umemtangaza aliyekuwa Kocha Mkuu wa timu ya Singida Black Stars, Mecky Mexime, kuwa kocha wao mkuu kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2024/25.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Johnson Fortnatus, alisema wameingia mkataba wa miaka miwili na kocha huyo kukinoa kikosi chao.

„Ni kweli leo (jana) tumemtangaza rasmi Mexime kuwa kocha wetu mkuu kwa ajili ya kuboresha benchi letu la ufundi kuelekea msimu wa 2024/25," alisema Fortnatus.

Katibu huyo alisema kocha huyo alisaini mkataba huo tangu Juni 10, mwaka huu na kudai ameahidi kuipa mafanikio makubwa kuelekea msimu ujao.

Alisema kwa sasa Mexime tayari amepokea ripoti iliyoachwa na aliyekuwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Francis Baraza, ili ajue ni wachezaji gani anaowaacha na watakaowasajili.

Alifafanua kuwa wameamua kumchukua kocha huyo baada ya kuridhishwa na utendaji wake wa kazi pamoja na uzoefu mkubwa aliokuwa nao kwenye kazi ya mpira.

„Baada ya kumalizana naye tumempa mikakati yetu ambayo ameahidi kuitekeleza lengo likiwa ni kuiweka mahali pazuri timu yetu," alisema.

Kwa upande wa Mexime alisema watahakikisha timu hiyo inashika nafasi ya juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

„Malengo yangu ni kuhakikisha ninapambania timu yangu ishike nafasi ya juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu msimu ujao, ninaomba mashabiki wangu wanipe ushirikiano," alisema Mexime.

**Winga wa Ureno, Francisco Conceicao, akishangilia baada ya kuifungia timu yake bao la kuongoza wakati ikishinda 2-1 dhidi ya Czechia kwenye mechi ya michuano ya Euro 2024 iliyopigwa Uwanja wa Red Bull Arena Leipzig, Ujerumani juzi usiku.** PICHA: MTANDAO



# JKU YANUKIA UBINGWA LIGI KUU Z'BAR

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

VINARA wa Ligi Kuu Zanzibar, JKU SC, wametanguliza mguu mmoja mbele kuukaribia ubingwa wa ligi hiyo baada ya juzi kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya KMKM SC.

JKU imejiweka katika nafasi hiyo nzuri baada ya mpinzani wake wa karibu Zimamoto SC kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Mlandege FC katika mchezo wao Ligi Kuu mzunguko wa 29.

Kwa matokeo hayo JKU sasa imefikisha alama 65 wakati Zimamoto ikifikisha pointi 62 huku kila moja imebakiza mchezo mmoja kufika tamati ya ligi hiyo.

JKU sasa inahitaji sare yoyote ili kutwaa ubingwa katika mchezo wake wa mwisho ambao itashuka uwanjani dhidi ya Kipanga FC leo katika Uwanja wa Amaan B.

Kwa upande wa Zimamoto ili kuupata ubingwa huo kwanza inatakiwa ashinde mchezo wake wa mwisho leo, lakini pia iwaombee wapinzani wao, JKU kupoteza mechi yao dhidi ya Kipanga.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Zimamoto, Mohmed Hilali, alisema mchezo wa mwisho wa Ligi Kuu Zanzibar ndio utakaoamua bingwa wa ligi hiyo.

Alisema bado wana nafasi moja ya mwisho ambayo katika soka lolote linaweza kutokea uwanjani, na kwamba kutoka sare katika mchezo wao muhimu hakujamvunja moyo wa ubingwa.

"Tunaendelea kupambana mpaka mchezo wa 30, hatupaswi kukata tamaa uwanjani kwa kuwa bado tupo katika njia ya ubingwa," alisema.

Upande wa timu moja ya kushuka daraja itakayoungana na timu tatu ambazo zimeshuka daraja tayar,i bado hali imezidi kuwa ngumu kutokana na Malindi SC kujiweka katika nafasi nzuri baada ya kutoka sare ya bila kufungana dhidi ya New City FC

Kwa matokeo hayo timu moja ambayo itaungana na timu tatu kushuka daraja bado haijajulikana kwani New City FC ina alama 34 na tayari imeicheza michezo 29, Kundemba FC yenye alama 29 imecheza michezo 28 na Hard Rock FC yenye pointi 30 imecheza michezo 28.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SIMONS AGOMBEWA
KLABU za Manchester United , Arsenal , Manchester City na Bayern Munich zote zimeonesha nia ya kutaka kumnunua mshambuliaji wa Uholanzi na Paris St-Germain, Xavi Simons mwenye umri wa miaka 21. ***(Mail)***

### OFA YA YORO YAKATALIWA
OFA ya Liverpool ya euro miloni 50 kumnunua mlinzi wa Lille, Leny Yoro mwenye umri wa miaka 18, imekataliwa. ***(Mundo Deportivo)***

### COLWILL HAKAMATIKI
JITIHADA za Bayern Munich kumnasa mlinzi wa Chelsea na England, Levi Colwill mwenye umri wa miaka 21, zimegonga mwamba, huku timu hiyo ya Ujerumani ikizingatia ada yoyote ya uhamisho wa nyota huyo kuwa juu sana. ***(Sky Sports Ujerumani)***

### IHEANACHO AFUATILIWA
KLABU ya Aston Villa inamfuatilia mshambuliaji wa Leicester City, Kelechi Iheanacho mwenye umri wa miaka 27, anapojiandaa kuondoka msimu huu wa majira ya joto kwa uhamisho wa bila malipo. ***(Football Insider)***

### MAATSE ANYATIWA
ASTON Villa pia inawasiliana kila siku na Chelsea kuhusu kutaka kumnunua beki wao wa pembeni, Ian Maatse mwenye umri wa miaka 22, ambaye yuko kwenye kikosi cha Uholanzi cha Euro 2024. ***(Football Insider)***

### CANCELO BEI JUU
MANCHESTER City hawatakubali dau la chini ya pauni milioni 25 kwa mlinzi wa Ureno, Joao Cancelo mwenye umri wa miaka 30, huku Barcelona wakiwa na nia ya kumsaini kwa mkataba wa kudumu baada ya muda wa mkopo. ***(Sun)***

### GREAVES KUMRITHI BRANTHWAITE
KLABU ya Everton inamtazama mlinzi wa Hull City, Jacob Greaves mwenye umri wa miaka 23, kama anayeweza kuziba nafasi ya beki wao wa kati, Jarrad Branthwaite mwenye umri wa miaka 21, ikiwa ataondoka msimu huu wa majira ya joto. ***(Hull Daily Mail)***

### DAVIES BADO BAYERN
KLABU ya Bayern Munich haijafanikiwa kukubaliana mkataba mpya na beki wa kushoto wa Canada, Alphonso Davies, ambaye amekuwa akihusishwa na Real Madrid, lakini hawana mpango wa kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 na kumruhusu kuingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake. ***(Sky Sports Ujerumani)***

### RODIN LULU SOKONI
KLABU za Ipswich , Southampton , Leicester na Leeds United ni miongoni mwa zinazotaka kumsajili mlinzi wa Wales na Tottenham Hotspur mwenye umri wa miaka 26, Joe Rodon. ***(Soka.London)***

### MATS AMULIKWA ROMA
AS Roma inalenga kumnunua beki wa Ujerumani, Mats Hummels mwenye umri wa miaka 35, ambaye kuondoka kwake Borussia Dortmund kumethibitishwa. ***(Calciomercato)***

### CALAFIORI ATAKIWA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur ni miongoni mwa zilizofanya mazungumzo ya awali kuhusu kumsajili beki wa Italia na Bologna, Riccardo Calafiori mwenye umri wa miaka 22. ***(CaughtOffside).***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO AWEKA REKODI MPYA MICHUANO EURO

Ni wakati akiendelea kushikilia ile ya kufunga mabao mengi, sasa awa...

**MUNICH,** UJERUMANI

CRISTIANO Ronaldo amekuwa mchezaji wa kwanza kushiriki michuano sita ya Ulaya wakati Ureno ilipoanza kampeni ya Euro 2024 kwa ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Jamhuri ya Czechia.

Mshambuliaji huyo alikuwa na mechi saba pekee kuelekea michuano yake ya kwanza ya Euro 2004, lakini aliingia katika michuano ya msimu huu wa majira ya joto akiwa na mechi zisizopungua 207 kwa nchi yake.

Hata hivyo, Ronaldo hakuweza kufunga bao katika mechi yake hiyo ya 208, huku Ureno walimiliki mpira kwa kiasi kikubwa.

Hii ilikuwa mara ya kwanza kwenye Euro 2024 kwa mchezo kutoka suluhu hadi mapumziko.

Francisco Conceicao aliyetokea benchi alifunga dakika za lala salama na kuipa timu ya Roberto Martinez ushindi.

Ronaldo alikuwa katikati ya mashambulizi mengi ya Ureno, akipita nafasi yao nzuri zaidi ya kipindi cha kwanza wakati alipochezeshwa na Bruno Fernandes na kuzimwa na kipa Jindrich Stanek aliyejitandaza kwa ustadi kuzima juhudi za mshambuliaji huyo.

Ronaldo alipiga shuti lingine kwa Stanek kabla ya mapumziko na mpira wa kichwa ukapanguliwa muda mfupi baada ya kuanza tena.

Akiwa kwa mara ya kwanza kwenye kikosi cha Ureno mwaka 2004, Ronaldo alicheza mechi yake ya kwanza ya Euro kwenye ardhi ya nyumbani, akifunga bao lake la kwanza katika michuano hiyo dhidi ya Czechia.

Sasa, miaka 20 baadaye, Ureno ilikabiliana na timu ileile katika mechi yao ya ufunguzi ya michuano ya sita ya Ronaldo.

"Leo inaanza sura nyingine katika historia yetu. Naikumbuka vema siku yangu ya kwanza na timu ya taifa, safari iliyojaa changamoto na ushindi. Sasa, nina heshima ya kuwa pamoja na timu ya mabingwa, iliyojaa vipaji na dhamira," aliandika Ronaldo katika chapisho lake kwenye mtandao wa X.

"Kwa nguvu na uungwaji mkono wa kila mtu, tunageuza ndoto kuwa ukweli. Hebu, pamoja, tupiganie ushindi mwingine."

Tangu alipocheza kwa mara ya kwanza 2004, Ronaldo ameshiriki katika kila timu ya Ureno iliyofuata - 2008, 2012, 2016, 2020 (iliyochezwa 2021 kwa sababu ya COVID-19) na sasa 2024.

Akiwa na mabao 14 ya Euro, Ronaldo anashikilia rekodi ya kuwa mchezaji aliyefunga mabao mengi zaidi katika historia ya mashindano hayo, huku rekodi yake binafsi ikiwa ni mabao matano katika kampeni moja katika mwaka 2020.

# MESSI AMTAJA RAMOS MPINZANI MKALI ZAIDI

**MIAMI,** MAREKANI

LIONEL Messi amesema Sergio Ramos ndiye alikuwa mpinzani wake mkubwa wakati wote wawili walipocheza El Clasico nchini Hispania.

Wawili hao walikuwa na vita nyingi wakati Messi alipoichezea Barcelona na Ramos akiongoza safu ya ulinzi ya Real Madrid.

Ushindani huo ulitulia wakati wawili hao bila kutarajia walipokuwa wachezaji wa Paris Saint-Germain mnamo 2021.

Akizungumza kwenye kipindi cha YouTube kuhusu ni mchezaji gani ambaye aligombana naye zaidi wakati wa uchezaji wake, Messi alisema: "Tulipigana sana na Sergio Ramos. Baadaye tukawa wachezaji wa timu moja, lakini kabla katika Clasicos, kila mara tulishikana, ilikuwa kali."

Hapo awali Ramos alimtaja Messi kama "mchezaji bora zaidi kuwahi kutokea."

Jumanne, kuondoka kwa Ramos kutoka Sevilla kulitangazwa na klabu hiyo ya Hispania.

Nahodha huyo wa zamani wa Hispania alirejea katika klabu yake ya utotoni msimu uliopita wa majira ya joto baada ya misimu miwili PSG na kufunga mabao saba katika mechi 37 alizochezea Sevilla.

Beki huyo mkongwe alikataa chaguo la kuongeza muda wake wa pili wa kusalia katika klabu hiyo, lakini akakanusha kuwa anafikiria kustaafu soka.

## Man City kufungua EPL na Chelsea msimu wa 2024/25.

**LONDON,** ENGLAND

MANCHESTER City itaanza kwa kuwa wageni wa Chelsea katika wiki ya kwanza ya msimu wa 2024/25 wa Ligi Kuu England.

Kwa upande wa Ipswich Town, ambayo ni miongoni mwa timu tatu mpya zinazojiunga na ligi hiyo, wataanza kwa kuwakaribisha Liverpool.

Hii ni mara ya kwanza kwa Ipswich kucheza Ligi Kuu baada ya miaka 22, ikitarajiwa kushuka uwanjani mnamo Agosti 17, 2024.

Lakini msimu huo utaanza na ufunguzi wa pazia la shindano hilo kwa mechi kati ya Manchester United na Fulham katika Uwanja wa Old Trafford Ijumaa ya Agosti 16.

Arsenal, waliomaliza katika nafasi ya pili kwenye ligi, watawakaribisha Wolverhampton katika Uwanja wa Emirates siku ya Jumamosi, huku Aston Villa wakisafiri kuelekea West Ham.

Southampton, ambao walirejea kucheza Ligi Kuu baada ya msimu mmoja kwenye Ligi ya Championship, watamenyana na Newcastle katika Uwanja wa St James' Park.

Everton watakuwa wenyeji wa Brighton huku Nottingham Forest na Bournemouth zikichuana siku ya Jumamosi.

Mechi zitakazochezwa Jumapili ya wiki ya kwanza ni pamoja na ile ya Brentford na Crystal Palace na mshindi wa Ligi ya Championship, Leicester City ambao watakuwa wenyeji wa Tottenham Hotspur Jumatatu ya Agosti 19.

Mara ya mwisho kwa Ipswich kushiriki Ligi Kuu ilichapwa mabao 5-0 na Liverpool kwenye Uwanja wa Anfield siku ya mwisho ya msimu wa 2001/02.

Mei mwaka huu, Manchester City ilitwaa ubingwa wa Ligi Kuu kwa mara ya nne mfululizo, baada ya kumaliza msimu uliopita ikiwa na pengo la pointi mbili kati yake na Arsenal waliokuwa wa pili katika jedwali.



## Mbappe kuikosa Uholanzi

**MUNICH,** UJERUMANI

KYLIAN Mbappe ataukosa mchezo unaofuata wa Ufaransa kwenye Euro 2024 baada ya kuvunjika pua kwenye mechi yao ya ufunguzi ya michuano hiyo dhidi ya Austria, vyanzo viliiambia ESPN.

Shirikisho la Soka la Ufaransa lilithibitisha kuwa mshambuliaji huyo alikwepa kuhitaji kufanyiwa upasuaji, jambo ambalo lingemfanya kuwa nje ya mashindano hayo. Badala yake atavaa mask maalum.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba atakuwa nje ya uwanja kwa ajili ya mchezo wao unaofuata - uliopangwa dhidi ya Uholanzi Ijumaa - licha ya awali Mbappe alitarajiwa kucheza.

"Kutakuwa na majaribio zaidi kuona jinsi mambo yanavyoendelea. Ni wazi ulikuwa mgongano mkubwa," alisema Kocha wa Ufaransa, Didier Deschamps."

Ufaransa haitaki kuchukua hatari yoyote kwa Mbappe ikizingatiwa atahitajika kwa muda wote wa mchuano huo, lakini anaweza kurejea dhidi ya Poland Juni 25 ikiwa itahitajika, ikiwa pua yake itahisi vizuri.

Ufaransa ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya wapinzani wa Kundi D Austria Jumatatu, na kuashiria mwanzo mzuri kwa kikosi cha Didier Deschamps huku kikifukuzia taji Hilo.

Mbappe, ambaye alipelekwa hospitalini huko Dusseldorf, Ujerumani, baada ya mechi, alichapisha kwenye mtandao wa kijamii: "Mawazo yoyote ya barakoa?"

Rais wa Soka Ufaransa (FFF), Philippe Diallo, aliuambia mkutano wa wanahabari Jumanne kwamba ana matumaini Mbappe atarejea haraka kwenye michuano hiyo

"Uliona, alikuwa na jeraha hili kwenye pua yake, habari hiyo inatia moyo," Diallo alisema. "Hakutakuwa na upasuaji katika muda mfupi. Kuhusu kurejea kwake, ni mapema leo kutoka ratiba; tutasubiri taarifa kutoka kwa daktari."

Kevin Danso, beki wa Austria ambaye aligongana na Mbappe, alituma ujumbe wa pole kwa fowadi huyo wa Ufaransa Jumanne.

"Namtakia ahueni njema na ninatumaini atarejea uwanjani haraka," aliandika Danso kwenye mtandao wa kijamii.

HABARI MICHEZO

# RUPIA, TCHAKEI WAGOMBEWA

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Singida Black Stars, imesema kuwa imepata ofa nyingi kutoka timu mbalimbali nchini zikiwahitaji wachezaji wake, straika Elvis Rupia, raia wa Kenya na kiungo mshambuliaji wa Togo, Marouf Tchakei.

Mkurugenzi wa Ufundi wa klabu hiyo, ambayo zamani ikiitwa Ihefu, Muhibu Kanu, amesema, mbali na wachezaji hao, pia kuna kiungo mkabaji, Yusuph Kagoma ambaye kuna timu inamhitaji.

"Kuna ofa nyingi mezani, nimeiona ya Rupia kuna watu wametuma barua ya kuleta ofa, zipo mezani kwangu nimeziona kuna wanaomhitaji Tchakei kuna timu inamtaka Yusuph Kagoma, yaani klabu zinataka wachezaji wetu tofauti tofauti," alisema Kanu.

Mkurugenzi huyo amesema hakuna mchezaji asiyeuzwa na klabu yoyote itakayofuata utaratibu, basi hawana matatizo, kwani na wao watakwenda kusaka wachezaji wengine bora zaidi.

"Kama ni kuondoka sawa, kwa sababu hakuna mchezaji asiyeuzwa, kinachotakiwa ni makubaliano ya timu mbili, tutauza wanaohitajika na klabu zingine na kupata dau nono, tutazuia wale ambao kocha atasema anawahitaji, na pia na sisi tutasajili kutoka klabu zingine," alisema.

Taarifa za ndani kutoka klabu hiyo zinaeleza Simba inawahitaji wachezaji wawili, ambao ni Kagoma ambaye tayari wameshamalizana na Wekundu wa Msimbazi, na sasa kinachosubiriwa ni dau kwenye klabu yake, na Tchakei ambaye ilimkosa kipindi cha dirisha dogo la usajili msimu uliomalizika.

Wakati huo huo, kikosi cha Singida Black Stars, kinatarajiwa kuanza maandalizi ya msimu mpya (pre season), Julai 3, mwaka huu.

Kanu, alisema uongozi umeshaweka malengo yake, ukitaka maandalizi ya msimu yaanze mwanzoni mwa mwezi ujao, huku ukimuachia kocha wake mpya, Patrick Aussems, kuchagua sehemu anayotaka kuweka kambi hiyo.

CHA PILI HICHO...



Winga wa Real Madrid, Arda Guler (jezi namba 8), akipongezwa na wachezaji wenzake wa Timu ya Taifa ya Uturuki baada ya kuifungia bao la pili wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Georgia, kwenye mechi ya michuano ya Euro 2024 iliyopigwa Uwanja wa Signal Iduna Park, Ujerumani juzi usiku. **PICHA: MTANDAO**

# Job amwangukia Morocco

Na Shufaa Lyimo

HATIMAYE beki wa timu ya Yanga, Dickson Job, amemuomba radhi Kocha wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Hemed Morocco, kutokana na utovu wa nidhamu aliouonyesha katika kikosi hicho jambo lililomsababisha kutoitwa kuitumikia kwenye mechi za kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia 2026.

Job anadaiwa alionyesha utovu wa nidhamu wa kugomea kucheza mechi katika michuano ya Afcon 2023 nchini Ivory Coast, kwa kile kinachoelezwa kuwa alifikia uamuzi huo kutokana na kupangwa nafasi ambayo hakuitaka.

Beki huyo kupitia pindi cha Kipenga Extra cha East Africa Redio na East Africa TV kwa mara ya kwanza amekanusha madai hayo yaliyofanya aonekane si mzalendo.

Amesema hajawahi kugomea mchezo wowote aliopangwa kucheza na kocha huyo, na kuhusishwa na kwamba taarifa hizo si za kweli.

Aidha, alitumia nafasi hiyo kumuomba radhi kocha wake Morocco pamoja na Watanzania ambao walikwazika kwa namna moja ama nyingine baada ya kusikia uvumi wa yeye kutokuwa mzalendo.

## Yanga: Tumewalipa waliotuburuza FIFA

INATOKA UK. 24

wahusika, na zuio hilo litaondolewa mara moja.

Kamwe, alikiri kuwa awali klabu hiyo ilikuwa imefungiwa kusajili kutokana na kutomalizana na wachezaji wao wa kimataifa, lakini si kwa sababu hawakuwa na pesa, au makusudi, ila walikuwa na kipaumbele kingine kwanza.

"Ni kweli katikati ya msimu huu tulifungiwa mara mbili, ya kwanza ilimhusu Mamadou Doumbia, ya pili Lazarous Kambole, wote walikuwa ni wachezaji wetu na kwa sababu za kimpira, tulishindwa kuendelea nao, ikatulazimu kuvunja nao mikataba, ni lazima uwalipe kwa mujibu mlivyokubaliana, baada ya hapo tukaweka kipindi cha kulipana, baadaye wakaenda FIFA na tukapangiwa kulipa madeni, tukafungiwa.

Wakati huo tulikuwa katikati ya mashindano, kama klabu kwa raslimali iliyokuwa nazo, tukaangalia vipaumbele muhimu kwanza, tunatakiwa kusajili au kutwaa makombe? Muda wa usajili bado, uongozi ukaona kipaumbele ni kupata makombe," alisema.

Pia, imekanusha taarifa za kudaiwa na Augustine Okra ikidai si sahihi na kwamba bado yupo kwenye kikosi hadi hapo taarifa zitakapotolewa baadaye.

Akizungumzia usajili, alisema inafanya usajili wa kishindo ambapo itaanza kuwapa mkono wa kwaheri wachezaji isiyowahitaji kuanzia Julai Mosi.

"Tumechelewa kutangaza tunaowaacha kwa sababu kuna klabu tumechukua wachezaji wao, lakini zinachelewa kuwapa barua za kuwaruhusu kuondoka, huwezi kutangaza kuwaacha watu bado huna uhakika wa kupata wengine, tunatarajia Julai Mosi tutaanza kutangaza 'thank you', alisema Ofisa Habari huyo.

## Jobe kwa mkopo, Chilunda apewa 'Thank You' Simba

INATOKA UK. 24

Ahmed alisema wanafanya mabadiliko makubwa kwa sababu wanataka kujenga Simba bora itakayotikisa msimu ujao.

"Bado sana, tunataka kutengeneza Simba bora zaidi, kwa hiyo tunaachana na wachezaji bora tuliokuwa nao, tunasajili bora zaidi ili twende tukafanye vizuri kwenye malengo ambayo tumejiwekea, hiyo ni asilimia mbili tu, safari hii panga ni kubwa mno, kuna wengine wanafuata mbele na kila utakayoona, mbadala wake atakuwa ni mchezaji wa kiwango cha juu.

"Fikiria kama unaweza kumuacha mchezaji kama Saido Ntibazonkiza ambaye hakuwa mchezaji wa benchi, alikuwa ndiye mfungaji bora wa klabu misimu miwili mfululizo, tafsiri yake ni kwamba maboresho yanayofanyika ni makubwa mno ndiyo maana klabu inapata uthubutu wa kuachana naye, safari hii hatutaki mchezo," alisema Meneja habari huyo.

Michezo

Nipashe Alhamisi Juni 20, 2024

## Ronaldo aweka rekodi mpya michuano Euro



UKURASA 21

EURO 2024...



Mshambuliaji wa Ureno, Cristiano Ronaldo, katika harakati za kuipambania timu yake kupata ushindi dhidi ya Czechia kwenye mechi ya michuano ya Euro 2024 iliyopigwa juzi usiku katika Uwanja wa Red Bull Arena Leipzig nchini Ujerumani na timu yake kuibuka na ushindi wa mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA: TUMEWALIPA WALIOTUBURUZA FIFA

## Yasema haidaiwi tena, yatangaza kuanza kutoa 'Thank You' Julai Mosi huku ikimtaja Okrah...

**Adam Fungamwango na Faustine Feliciane**

KLABU ya Yanga imesema imeshamalizana na wachezaji wote wanaoidai, hivyo wako huru kusajili, ikitangaza kuwa Julai Mosi, mwaka huu, itaanza kuwapa mkono wa kwaheri wote ambao haiwahitaji kuelekea msimu ujao.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema siku moja tu kabla ya dirisha la usajili kufunguliwa, walimalizana na wachezaji wao Mamadou Doumbia na Lazarous Kambole na kupokea barua pepe kutoka Shirikisho la Kimataifa la Mpira wa Miguu Duniani (FIFA) wakithibitisha kupokea vithibitisho vyote vya malipo.

"Dirisha lilifunguliwa Juni 15, lakini siku moja kabla ya kufunguliwa tulikuwa tumeshamaliza kulipa kila kitu, kwa maana ya madeni yote ya wachezaji hao, juzi tumepokea barua pepe kutoka FIFA, wakithibitisha kuwa tayari wamepokea vithibitisho na viambatisho vya malipo, ilikuwa inawasiliana na wachezaji, wamewasiliana na Doumbia ila bado Kambole hawajampata na wametoa siku tano.

"Kama hawajawasiliana naye, basi wataturuhusu, kusajili, hivi ninavyozungumza hatuna kesi yoyote FIFA mpaka sasa inayohusu Klabu ya Yanga, tumshamaliza kila kitu," alisema Kamwe.

Alikuwa akitoa ufafanuzi, baada ya Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), kutoa taarifa ya kufungiwa kwa timu hiyo, pamoja na zingine nne, ambazo ni Singida Fountain Gate, Tabora United, Biashara United na FGA Talents, hadi pale zitakapowalipa wachezaji wanaozidai.

TFF ilidai kuzizuia klabu hizo ikishirikiana na FIFA, hadi pale zitakapowalipa

INAENDELEA UK. 23

## Jobe kwa mkopo, Chilunda apewa 'Thank You' Simba

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikimpa mkono wa kwaheri mchezaji, Shaaban Chilunda, Klabu ya Simba inatarajiwa kumtoa kwa mkopo straika wake, Pa Omari Jobe, raia wa Gabon aliyesajiliwa katikati ya dirisha dogo la usajili msimu uliomalizika, baada ya kiwango chake kutowaridhisha wanachama na mashabiki wa klabu hiyo.

Taarifa kutoka ndani ya klabu ya Simba zinaeleza kwa sasa juhudi zinafanyika kumtoa kwa mkopo mchezaji huyo kwenda timu yoyote ile, ndani au nje ya nchi, ili nafasi yake ichukuliwe na mchezaji ambaye atakuwa na tija ndani ya kikosi.

Habari zinadai, Simba imeshindwa kuvunja mkataba na mchezaji huyo iliyomsajili kwa mwaka mmoja na nusu kwani itapaswa kumlipa kiasi cha Sh. milioni 200 za Kitanzania, kitu ambacho kimewawia vigumu mabosi wa klabu hiyo.

"Jamaa aliingia mkataba wa mwaka mmoja na nusu, ufanisi wake haujawaridhisha, viongozi walitaka kuvunja mkataba, lakini pesa ni nyingi anazotakiwa kulipwa, na haiwezekani kubaki, sidhani kama kuna mwanachama au shabiki wa Simba anaweza kuwaelewa viongozi Jobe akibaki.

"Kwa hiyo anatafutiwa timu aende kwa mkopo ili ipatikane nafasi ya kusajili straika mwingine, na kwa bahati nzuri klabu mbalimbali ndani na nje ya nchi zinamhitaji, hivyo itakuwa rahisi tu," kilisema chanzo hicho.

Wakati hayo yakiendelea, klabu hiyo imetangaza kuachana na straika, Shaaban Chilunda, ambaye alikuwa anacheza kwa mkopo katika Klabu ya KMC.

Katika kampeni yake ya kutangaza wachezaji inayowaacha kila siku mchana, Simba imeachana na Chilunda aliyesajiliwa mwanzoni mwa msimu akiwa hana timu, ingawa awali alikuwa akikipiga katika Klabu ya Azam FC.

Baada ya kutoonyesha kiwango cha kuridhisha, klabu hiyo ilimpeleka KMC kwa mkopo ambako amecheza mpaka mwisho wa msimu uliomalizika.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema bado kuna wachezaji wengi sana wataachwa ikiwa ni kampeni ya kutengeneza Simba mpya.

Akizungumza jijini Dar es Salaam,

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002